# Nipashe

Jumanne Desemba 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581515

nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US | nipasheTZ | The Nipashe Digital | nipasheTZ | nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




UKURASA 22

**NIMEPATA FURAHA KUIFUNGA ATLETICO**

MAAFA MANYARA

# Kijiji chafunikwa tope na magogo

• **Kanisa** labaki, babu asimulia alivyonusuru wajukuu wanne, mkwe; mzee mwenzake aokoa mke, watoto... *Endelea Uk. 2&3*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua maeneo yaliyoathirika na mafuriko katika Kijiji cha Gendabi wilayani Hanang' jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

UKURASA WA 4

**Shirika** Nyumba, CRDB zaingia ubia mradi wa kuuza nyumba Z'bar



UKURASA WA 5



**Sabaya** Mwenyekiti mpya CCM Arusha

UKURASA WA 5

**Moto** wateketeza nyumba, hakuna kilichookolewa



## Janga la radi laua watu sita Mtwara

UKURASA 4



## ...Vifo vyaongezeka, Rais Samia aelekeza serikali kubeba msiba

• **Wataalamu** wakosoa utayari kukabili majanga...

**MICHEZO** **BENCHIKHA AAHIDI KUIBADILI SIMBA SC** UK.24 **KATUNI** UK.6

MAAFA MANYARA

# Kijiji chafunikwa tope, mawe; waliofikwa wafunguka mateso

**Na Jaliwason Jasson,**
HANANG'

UKIFIKA katika Kijiji cha Gendabi, wilayani Hanang', mkoani Manyara kwa sasa, ni vigumu kuamini kwamba kilikuwa na makazi ya watu zaidi ya 2,000 katika vitongoji vyake vitano.

Kinachoonekana sasa kwa macho kijijini huko ni miti, magogo, mawe na tope; si eneo linalofaa kwa makazi ya binadamu tena.

Ni maafa yaliyoacha simanzi kubwa na historia isiyofutika ya kupoteza zaidi ya watu 63 kutokana na tope lililoporomoka toka Mlima Hanang', mmoja wa wakazi wake, akisimulia alivyopoteza wajukuu wanne na mama yao.

Aidha, Nipashe ilifahamishwa kwenye eneo la tukio kwamba hadi jana jioni, majeruhi waliopelekwa katika hospitali na vituo vya afya, ni zaidi ya 80.

Katika maafa hayo, Mkazi wa Kijiji cha Gendabi, Petro Mjeni (75), ameeleza namna alivyoshuhudia tope likiporomoka kutoka mlimani lilivyosababisha vifo vya wajukuu zake wanne na mama yao, baada ya kuzingirwa na tope hilo.

Akisimulia maafa hayo yalivyoacha simanzi kubwa katika familia yake, Mjeni alisema jana, "sina cha kusema zaidi ya kuomba rehema ya Mungu. Watoto wanne wa kijana wangu, wote na mke wake hawapo, wamekufa, lakini kijana wangu yeye alijiokoa na yuko mahututi hospitalini.

"Mimi ninakaa upande wa pili wa juu (kuelekea Mlima Hanang'). Haya mafuriko yalinikuta nikiwa kule juu, nikasikia kelele watu wanapiga nikajitokeza nikaja hapa nyumbani kwa kijana wangu, ilikuwa majira ya saa 12 asubuhi (juzi).

"Nilipofika hapa nikashangaa, nikasema 'Mungu wangu!' Sasa hata mawasiliano sina."

Wakati Petro akipoteza wapendwa wake hao, jirani yake, Samwel Samson, mkazi wa Gendabi (69), naye amesimulia alivyookoa mke wake, mwanawe na mtoto wa shemeji yake toka kwenye mafuriko hayo ya tope.

Samson (69) anasema alifanikiwa kuiokoa familia yake baada ya kukimbilia kwenye nyumba ya urithi aliyoachiwa na baba yake.

"Nyumba hii unayoiona, ni nyumba ya kwangu ambayo nimeachiwa urithi na baba yangu, lakini nyumba yangu kabisa niliijenga hapa miti unapoiona. Imefutika kabisa kabisa, haionekani!

"Sasa ninachokikumbuka ni kwamba, usiku wa kuamkia jana Jumapili (Desemba 3, 2023), mimi nilikuja nikalala kwenye hii nyumba ya urithi kwa sababu nilikuwa ninajiandaa kwa ajili ya ibada kanisani.

"Sasa, ilipofika asubuhi saa 11:30, nikatoka ili niweze kuendelea na maandalizi mengine, nikasikia mngurumo kama wa gari, nikatoka kwenda barabarani kuangalia kwa sababu nyumba yangu iko karibu na barabara.

"Nilipoona ni maji yanapita barabarani, sikujali sana. Nikarudi ndani. Nilipofika ndani, nikasikia sasa mngurumo mkubwa kama tetemeko. Kumbe ni mawe yalikuwa yanaviringika kutoka huko mlimani!

"Kutazama vizuri, nikaona mbona yale mawe yanakuja niliko na nyumba za jirani zangu zinaanguka? Nikakimbia haraka kule alikokuwa mke wangu amelala, nikamchukua mke wangu, mtoto wangu na mtoto wa shemeji yangu, ambaye tunakaa naye. Tukatoka tunakimbia ili kuja kwenye hii nyumba (anaonesha aliko).

"Nikifikiri kwamba tumekuja kwenye hii nyumba tutakuwa salama, lakini tulipofika hapa niliona mawe makubwa na tope yanalenga kuja tulipo. Tulishuhudia majengo yanaanguka," anasimulia.

**HATUA SERIKALINI**

Wakati Rais Samia Suluhu Hassan amekatiza ziara yake Dubai alikokuwa kwenye mkutano wa mazingira duniani (COP28) kurejea nyumbani, ameagiza serikali ibebe mzigo wa kugharamia maziko na kuwahudumia waathirika wa janga hilo.

Katika maelekezo yake, Rais amesema majeruhi wote waliopelekwa hospitalini kupata matibabu, wapate huduma hiyo kwa gharama ya serikali.

Mara baada ya tukio hilo juzi, Rais Samia Dubai, alielekeza Kamati ya Kitaifa ya Maafa kufikia huko mara moja, kuungana na hatua za dharura zilizokuwa zinaendelea.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendega, Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ) nalo lilifika mahali huko tangu juzi usiku na kuanza kazi mara moja ya uokoaji.

Vilevile, mbali na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anayeiongoza timu ya uokoaji, pia wamo viongozi wengine wa ulinzi na usalama, akiwamo Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillius Wambura.

Rais Samia katika maelekezo yake, amekiagiza Kitengo cha Maafa cha Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhakikisha wananchi wote ambao makazi yao yamesombwa na maji, wapatiwe mbadala wa makazi ya muda kujisitiri kwa sasa.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa Ikulu, maeneo yaliyoathiriwa na maafa hayo ni ya mji wa Katesh na vitongoji vyake, hususan vijiji vya Jorodom, Ganana na Dumbeta, pia vijiji vya Gendabi, Sarijandu, Arukushay na Sebasi.

Taarifa ya awali inaonesha pia nyumba na mifugo vimeathirika, huku idadi za kaya zilizoathirika ni wastani 1,150; idadi ya watu walioathirika ni 5,600 na inakadiriwa takriban ekari 750 za mashamba zimeharibika.

Kwa mujibu wa mwandishi wa Nipashe aliyoko eneo la tukio, wakati uokoaji unaendelea, unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo barabara kuharibika, zikiwa na tope, magogo na mawe yanayokwaza mawasiliano katika hekaheka za uokoaji.

Kuhusu uharibifu, Rais Samia ambaye pia alitanguliza pole kwa waliofikwa na madhara hayo, ameagiza mamlaka za kiserikali kufanya tathmini ya kina ya mkasa huo, ikienda sambamba na juhudi za ziada usiku na mchana kurejesha eneo hilo katika hali ya kawaida.

***Taarifa za ziada na Godfrey Mushi (ARUSHA)**



Wakazi wa Kijiji cha Gendabi Katesh mkoani Manyara wakisafisha barabara iliyofunikwa na tope baada ya mvua kubwa iliyonyesha Jumapili na kuharibu nyumba na miundombinu mbalimbali jana. **PICHA: JALISWASON JASSON**

Kamal

KAMAL GASES LIMITED

TAARIFA KWA UMMA

Sisi **Kamal Gases limited** wazalishaji namba moja wa gesi za viwandani zenye ubora uliothibitika na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Tumegundua kuwepo kwa wazalishaji wa gesi wanaotumia mitungi yenye nembo ya KGL kinyume na sheria.

Tunawatangazia wazalishaji, watumiaji wa gesi za viwandani na umma kwa ujumla kwamba ni kinyume cha sheria kujaza, kuuza, na kusambaza gesi iliyowekwa kwenye mitungu yenye nembo ya kamal ambayo haikuzalishwa na Kamal Gases Limited.

Hivyo mnahabarishwa kwamba; Kamal Gases Limited wapo katika zoezi kabambe la kufuatilia na kukamata wahusika wote wanaozalisha gesi za viwandani na kujaza katika mitungi yenye nembo au alama ya kamal gases limited kinyume cha utaratibu.

Kamal Gases Limited itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungua kesi za madai na jinai kwa yoyote atakaye tumia mitungi ya gesi yenye nembo ya Kamal Gases Limited kujaza gesi aliyoichakata mwenyewe au iliyochakatwa na wazalishaji wengine nje ya Kamal Gases Limited

Tunatoa wito kwa wateja wetu kuendelea kutumia huduma ya gesi ya Kamal Gases Limited kwa kupitia vituo vilivyoidhinishwa na kuitambulika na Kamal Gases Limited au wafike kiwandani chang'ombe industrial area plot no. 188/2 kwa maelezo zaidi piga simu namba **+255 765 169 444**

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kamal Gases Limited**
**Dar es Salaam**

21769080Z

MAAFA MANYARA

# Wadau wakosoa utayari uokoaji katika majanga

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imepeleka chopa tatu za uokoaji na vikosi mbalimbali vya askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuongeza nguvu ya kuokoa watu walionasa katika tope lililoporomoka katika Mlima Hanang'.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza jana wakati wa kutambua na kuaga miili ya waliofariki dunia kwamba, hadi jana saa 12 jioni, maporomoko hayo yamesababisha vifo vya watu 63 na wengine zaidi ya 116 wamejeruhiwa. Kati ya waliofariki dunia, 40 ni wanawake.

Majaliwa alisema katika kijiji cha Gendabi karibu nyumba zote zimefunikwa na tope. Kanisa limenusurika.

Baadhi ya wataalamu wa majanga nchini na wanasiasa wametoa salamu za rambirambi, huku wakikosoa utayari wa nchi kukabiliana na majanga ya asili.

Kabla ya Rais Samia Suluhu Hassan kuelekeza serikali kuongeza nguvu katika uokozi, shughuli za uokozi katika siku ya kwanza zilikuwa zinafanyika kwa kutumia kamba, kuvuta miili ya walipoteza maisha wakiwa kwenye makazi yao.

Mtaalamu Mbobezi na Mhandisi wa Majanga nchini, James Mbatia, akizungumza na Nipashe jana, alisema "majanga ya asili duniani leo ni asilimia nne ya majanga yote, na asilimia 96 ya majanga yanasababishwa na binadamu.

"Hili janga lililotokea Hanang' kwa kiasi kikubwa ni majanga yaliyotengenezwa na binadamu na si majanga asilia. Sasa tufanye nini kwa sasa hivi? Ningeshauri kutokana na hali hii tete iliyopo, serikali ikubali haina vifaa vya kisasa vya uokoaji.

"Kwahiyo, kunatakiwa kuwapo nguvu kubwa ya kuangalia sasa maeneo yote, ambayo ni hatarishi kibinadamu waondolewe huko kwa sababu gharama ya uhai wa binadamu ni kubwa kuliko kitu chochote kile.

"Hebu tuweke akili zetu chini tuone kwamba tuko tayari kihimili majanga? Tulipambana na hili jambo tangu mwaka 2010 na mwaka 2015 tukatunga sheria, ikatiwa saini na Rais Jakaya Kikwete Mei 11, 2015.

"Japo hii sheria ilifanyiwa marejeo katika serikali iliyopita, lakini ilikuwa inataka serikali iwe na wakala anayejitegemea wa kusimamia majanga, kama ilivyo TARURA au TANROADS. Ni sheria tunayo, ilitungwa bungeni lakini mpaka leo hii wakala haujaanzishwa."

Kwa mujibu wa Mbatia, Sheria hiyo Na. 7 ya Mwaka 2015 inaelekeza utayari wa kukabili majanga unapaswa kushuka mpaka kwenye ngazi ya kitongoji, lakini kuwapo na wakala unaojitegemea.

**KAULI CHADEMA**

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, alisema jana kuwa chama kimehuzunishwa na taarifa ya vifo na majeruhi vilivyosababishwa na mafuriko hayo.

"CHADEMA Kanda ya Kaskazini tumefuatilia kwa karibu tukio hili la mvua kubwa iliyonyesha na kushuka kutoka Mlima Hanang' ikiwa imebeba tope zito, miti, magogo na mawe na kisha kuleta madhara makubwa ya maisha ya watu, mali na miundombinu katika mji wa Katesh na maeneo kadhaa ya Wilaya ya Hanang'.

"Jambo hili linahitaji jitihada za pamoja za kizalendo kwa kutoa na kufikisha misaada kwa waathirika na faraja kwa familia zilizopata misiba sambamba na kurejesha hali ya miundombinu katika unafuu kwa kipindi hiki," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema wako katika eneo hilo kusaidiana na serikali kutoa msaada kwa waathirika, pia kuchunguza chanzo cha mafuriko hayo ili kufahamu namna wanavyoweza kuzuia yasitokee tena.

Meneja wa Kukabiliana na Maafa wa Shirika la Msalaba Mwekundu, Samwel Katamba, aliiambia Nipashe jana kuwa wanashirikiana na serikali kutoa huduma ya kwanza na msaada kwa waathirika ikiwamo maturubai, magodoro, mashuka na nguo.

Alisema pia wanatoa huduma ya afya kwa majeruhi na msaada wa kisaikolojia kwa walioathirika kwa namna yoyote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema wamesikitishwa na tukio hilo ambalo limekatisha uhai wa watu, akisisitiza hakuna mtu wa kumtupia lawama kwa kuwa ni janga la asili.

Alishauri mamlaka za serikali na kamati zinahusika kutoa msaada, zifanye kazi zake kwa haraka na weledi ili kuepuka kutokea vifo zaidi na kutoa misaada ya hali na mali kwa waathirika ili kuwatia moyo na matumaini.

Mtaalamu Mbobezi wa Jiolojia na Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST), Dk. Dalali Kafumu, alisema walitegemea kuwa kadri mvua ya El-Nino inavyoendelea kuimarika, inaweza kusababisha madhara katika maeneo tofauti.

Alisema kunapokuwa na ongezeko la joto juu ya wastani katika eneo la kati la Bahari ya Pasifiki, kunakuwa na tabia ya ongezeko la mvua katika meneo mengi ya ukanda wa Afrika Mashariki ikiwamo Tanzania, yanayoweza kulata madhara.

Alisema kutokana na hali hiyo, wamekuwa wanatoa elimu kwa jamii ili ichukue tahadhari inayoweza kutokana na ujio wa mvua hiyo ili kuepuka madhara mengi ikiwamo mafuriko, kuharibika miundombinu na vifo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Alli Mwinyi, alisema jana amepokea kwa masikitiko na mshtuko taarifa za mafuriko na maporomoko hayo.

Rais Dk. Mwinyi alisema anaungana na Rais Samia Suluhu Hassan kutuma salamu za pole kwa wananchi wa Mkoa wa Manyara kufuatia maafa hayo.

Katika hatua nyingine, kampuni za mawasiliano nchini zimetoa Sh. milioni 240 kwa ajili ya kusaidia waathirika waliokumbwa na mafuriko hayo.

Kampuni hizo zilitoa msaada huo jana jijini Dar es Salaam na kuukabidhi kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Mwenyekiti wa Umoja wa Shirikisho la Kampuni za Simu Tanzania (TAMNOA), Philip Besiimire, alisema kampuni za simu zimeona kilichotokea Manyara, hivyo hazina budi kuungana kuisaidia serikali kwa ajili ya waathirika.

***Imeandaliwa na Jaliwason Jasson (HANANG'), Jenifer Gilla, Halfani Chusi (DAR) na Godfrey Mushi (ARUSHA)**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

## TANGAZO KWA UMMA

**KUSAINI MIKATABA YA MALIPO YA FEDHA ZA KUSAIDIA KUPATA ARDHI MBADALA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Serikali, kupitia tamko la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI la tarehe 15/11/2023, imeamua kuwalipa waathirika wote wanaohamishwa malipo sawa kwa ajili ya kuwasaidia kupata ardhi mbadala. Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo sawa kwa ajili ya kupata ardhi mbadala kwa waathirika wote ambao wameafiki malipo yao katika zoezi la mwezi Oktoba 2023. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata na Mtaa kwa ratiba ifuatayo:

| KATA | MITAA INAYOHUSIKA | TAREHE |
|---|---|---|
| Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 6 hadi 7/12/2023 |
| | Misheni Kota<br>Ilala Kota | 8 hadi 9/12/2023 |
| Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| Upanga Magharibi | Charambe | 10 hadi 11/12/2023 |
| Jangwani | Mtambani A<br>Mtambani B | |
| Magomeni | Suna | 12 hadi 14/12/2023 |
| Mzimuni | Idrisa<br>Mtambani<br>Mwinyi Mkuu | |
| Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 15 hadi 16/12/2023 |
| Hananasifu | Mkunguni A<br>Mkunguni B<br>Hananasifu | |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

# Janga la radi laua sita wakiwa kwenye sherehe

**Na Hamis Nasir,** MASASI

WATU sita wakazi wa Kijiji cha Maparagwe, Kata ya Chikukwe, wilayani Masasi mkoani Mtwara, wamefariki dunia na wengine watano kujeruhiwa baada ya kupigwa radi wakati wakiwa wamekusanyika kwenye sherehe ya ngoma za unyago na mpeano katika kijiji hicho.

Tukio hilo lilitokea jana katika Kijiji cha Maparagwe majira ya saa 12:30 jioni wakati wananchi hao wakiwa katika sherehe hizo na ghafla mvua iliyoambatana na upepo pamoja na radi kuwapiga. Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni, alifika katika eneo la tukio na kutoa pole kwa wafiwa kwa niaba ya serikali.

Kanoni alisema serikali imepokea kwa masikitiko vifo hivyo na inaungana pamoja na ndugu na familia za wafiwa hao.

Alisema kutokana na vifo hivyo serikali imeahidi kugharamia shughuli zote za mazishi ikiwamo gharama za majeneza.

Mkuu huyo alisema serikali inatoa rai kwa wananchi kuacha kukusanyika kipindi cha mvua kuepuka matukio kama hayo.

Alisema majeruhi hao watano wamelazwa katika Hospitali ya Misheni ya Ndanda na serikali pia itagharamia fedha zote za matibabu.

Kadhalika, waliofariki katika tukio hilo ni wanawake watano na mwanaume mmoja huku majeruhi waliolazwa wanawake ni watatu na wanaume wawili.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Ndanda, Scristiani Kihando, alisema alipokea miili ya watu sita waliofariki baada ya kupigwa na radi.

Alisema hali za majeruhi zinaendelea vizuri kwa kupatiwa matibabu.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Maparagwe, walisema wamepokea kwa masikitiko tukio hilo.



Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Tanzania Commercial Bank Plc (TCB), Adam Mihayo (kulia), akizungumza baada ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Edmund Mndolwa (kushoto), kumtambulisha rasmi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZHC, CRDB zaingia ubia uuzaji nyumba kwa wananchi Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba la Zanzibar (ZHC) limeingia makubaliano na Benki ya CRDB kuwezesha wateja wa makundi mbalimbali kumiliki nyumba katika miradi inayosimamiwa na shirika hilo visiwani Zanzibar.

Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo wakati wa hafla iliyofanyika ofisi ya benki huko Michenzani, Mkurugenzi Mkuu wa ZHS, Mwanaisha Ali Said, alisema makubaliano hayo yatawawezesha kukamilisha vyema nyumba hizo sambamba na kuipongeza benki hiyo kwa kuendeleza ushirikiano huo.

Alisema fursa hiyo itaongeza ufanisi wa kazi katika miradi mipya inayotarajiwa kufanyika kupitia njia ya malipo ya taslimu, kulipa kwa awamu na njia ya mkopo.

Mwanaisha alisema njia ya mkopo ilikuwa haijafanya vizuri, hivyo kwa kufikiwa kwa makubaliano hayo, shirika litawasaidia kupata wateja katika njia ya tatu, yaani kwa wateja kupata mikopo.

Hivyo, makubaliano hayo Mwanaisha alisema yatagusa miradi yote inayotarajiwa kujengwa na wana mpango kujenga maeneo ya Nyamanzi na kuwataka wananchi kupeleka maombi yao.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili, alisema makubaliano hayo yatakwenda kuwanufaisha wateja wa makundi mbalimbali kwa kupata mkopo wa thamani ya hadi Sh. bilioni moja.

Alisema makundi hayo ni pamoja na wafanyakazi wa mashirika au taasisi, wanachama wa mifuko ya pensheni, wajasiriamali waliojiajiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, Watanzania wanaoishi nje ya nchi (diaspora) na Watanzania waishio nje ya nchi wanaomiliki hati za kusafiria za nchi nyingine. Alisema kutiwa saini kwa makubaliano hayo ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo katika kuwawezesha Watanzania kumiliki makazi bora.

Mkuu huyo alisema benki hiyo ndio kinara wa utoaji wa mikopo ya nyumba, akifafanua kuwa kati ya mikopo yenye thamani ya takribani bilioni 593.76 iliyotolewa na taasisi za fedha, CRDB imetoa takribani Sh. bilioni 197.70 sawa na asilimia 33.3.

Hivyo, alisisitiza kuwa benki itaendelea kushirikiana na ZHC kwa kufanya nao kazi, akilipongeza shirika hilo kwa kazi nzuri linayoifanya katika kuboresha hali ya makazi visiwani Zanzibar.

Adili pia alipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa utekelezaji na ufanikishaji wa miradi hiyo ya uongozi wa awamu ya nane ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kukuza hali ya makazi ya wananchi wa Zanzibar.

"Na sisi tunaungana naye katika jitihada hizi kwa kuhakikisha tunawawezesha wananchi wa Zanzibar na duniani kote kumiliki makazi bora kwa gharama nafuu," alisema.

Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Zanzibar, Abdalla Duchi, alisema benki yao itaendelea kufanya kazi na serikali na taasisi mbalimbali ili kuona wananchi wanapata maendeleo kupitia benki hiyo.

## Serikali yaeleza utayari wake kukabili usonji, mtindio ubongo

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali imeeleza utayari wake katika kuongeza juhudi zaidi kushughulikia changamoto ya usonji na utindio wa ubongo kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitalini ili kusogeza huduma na uelewa wa jamii kuhusiana na usonji.

Pia imethibitisha mpango wake wa kuingiza masomo ya elimu jumuishi na lugha za alama kwenye mtaala wa ualimu kuanzia mwakani ili kuwajengea uwezo wa kutosha walimu kuhusu namna bora ya kuwasadia wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Dhamira hiyo ya serikali ilielezwa jana na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel na Mkurugenzi wa Elimu Maalum Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya wakati wa kuhitimisha mkutano wa kimataifa wa siku mbili uliolenga kujadili changamoto zinazohusiana na hali ya usonji na mtindio wa ubongo uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo uliandaliwa kwa ushirikiano baina ya taasisi ya Victorious Centre of Excellence na Autism Connect.

Victorious Centre of Excellence ni kituo kinachotoa huduma mbalimbali za tiba ya urekebishaji na shughuli za ziada kwa watoto wenye hali ya usonji nchini kwa lengo la kuwajumuisha katika jamii. Autism Connect ni taasisi ya kimataifa iliyojikita kwenye kueneza ufahamu, kutoa elimu na kuwezesha utunzaji wa kina kwa watu wenye hali ya usonji kwa nchi mbalimbali duniani.

Akizungumzia utayari wa serikali katika kuongeza juhudi zaidi kwa ajili ya kushughulikia changamoto za usonji na mtindio wa ubongo kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali, Naibu Waziri Mollel aliwaomba wataalam wa afya walioshiriki kwenye mkutano huo kuandaa mapendezo muhimu yatakayoiongoza serikali kutekeleza azma hiyo kwa haraka zaidi.

"Jambo zuri zaidi kuhusu mkutano huu ni kwamba umewakutanisha wataalam wengi zaidi, tena kutoka mataifa mbalimbali yakiwamo yalioyopiga hatua katika nyanja hizi za changamoto ya usonji na mtindio wa ubongo ikiwamo nchi ya India.

"Ni matumaini yangu watatupa ushauri mzuri kuhusu namna bora ya kufanikisha dhamira hii ya serikali," alisema Dk. Mollel.

Aliwataka wazazi nchini kuacha tabia ya kuwaficha watoto wao wenye hali ya usonji na mtindio wa ubongo, bali wawekeze nguvu zaidi katika malezi sahihi ya watoto kwa kutambua zaidi mahitaji na haki zao za msingi ikiwamo kupatiwa elimu stahiki, kufanyishwa mazoezi ya kiafya na kiakili na kuepushwa na unyanyapaa wa aina yoyote.

Akizungumzia mpango wa kuingiza masomo ya elimu jumuishi na lugha za alama kwenye mtaala wa ualimu kuanzia mwakani, Dk. Matonya alisema hatua imeshakamilika na inalenga kuwajengea uwezo wa kutosha walimu kuhusu namna bora ya kuwasadia wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali waliopo shuleni.

Mkurugenzi wa Victorious Centre of Excellence ambaye pia ni Mwenyekiti wa mkutano huo, Sarah Laiser na Mwenyekiti Mtaalam wa taasisi ya Autism Connect, Dk. Nandini Gokulchandran walisema washiriki wamepata fursa kubadilishana mawazo na matokeo ya kimatibabu huku ukiwashirikisha wazazi wa watoto wenye hali ya usonji.

# Moto ulivyoteketeza nyumba ya familia 6

Na Christina Mwakangale

FAMILIA sita zilizokuwa zinaishi katika nyumba ya kupanga mtaa wa Mkoroshini-Kisondo, Mombasa, Ukonga jijini Dar es Salaam, zimenusurika baada ya moto ulioanza majira ya asubuhi kuteketeza mali zao ikiwamo fedha zilizohifadhiwa kwenye vibubu.

Tukio hilo limetokea jana, saa mbili asubuhi, huku baadhi ya wapangaji wakisema chanzo cha moto huo, kilianzia sehemu inayounganisha umeme kutoka nje kuingia ndani ya nyumba.

Nipashe ilishuhudia tukio hilo, saa chache baada ya ajali hiyo kutokea, ilikutana na maofisa wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakishirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Uokoaji na Zimamoto, kusaidia kuuzima moto huo.

Miongoni mwa wapangaji sita, waliokuwa wamepanga katika nyumba hiyo, Amina Kimolo, alisema tukio lilipotokea alikuwa nje pamoja na majirani zake, akifanya usafi huku watoto wake wakiwa ndani wamelala.

"Muda mfupi nikaona moshi unatoka chumba cha jirani, kurudi ndani nakuta moshi unaongezeka nikatoka haraka kuwatoa watoto," alisema Amina.

Mama Juma, ambaye naye muathiriwa katika tukio hilo, alisema moto ulianzia nje wa ukuta wa chumba chake, huku mtoto wake mdogo akimtaka aende nje kushuhudia moshi unapotokea.

"Mwanangu mdogo aliniita nje akasema mama mama kuna moto unawaka pale pakuwekea Luku ya umeme, kutoka nje ni kweli. Nikarudi ndani labda nianze kuwahi kutoa vitu moto ukazidi tayari kwenye mbao za paa.

Mpangaji mwingine ambaye hakuwa tayari kutaja jina lake, kutokana na majonzi aliyonayo huku akibubujikwa na machoizi alisema: "Kila kitu kimeungua nimabaki mimi kama nilivyo.

"Ndani nilikuwa nimeweka Sh. 560,000 nazo zimeteketea, kilichobaki ni mtungi tu wa gesi ndogo, kila ninapofikiria na kutazama sipati majibu," alisema binti huyo.

Aidha, wapangaji wengi wa nyumba hiyo, walisikitika kupoteza mali zao hususan fedha ambazo, zilizihifadhi katika kibubu, huku mwingine pia akidai alikuwa na Sh. 400,000 kabla ya tukio hilo.

Mjumbe wa nyumba 10, Elitruda Njau, alisema alipata taarifa ya tukio hilo asubuhi na alipowasili eneo la ajali, alishirikiana na wananchi kuuzima moto kwa kutumia ndoo zilizokuwa zimehifadhi maji kutoka kwa majirani.

## Sabaya Mwenyekiti mpya CCM Arusha

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

ALIYEWAHI kuwa Mkuu wa Wilaya za Songea, Serengeti na Mtwara kwa nyakati tofauti, wakati wa utawala wa hayati Rais Benjamin Mkapa, Thomas Sabaya, 'ameula' baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM, Mkoa wa Arusha.

Sabaya, aliibuka mshindi wa kiti hicho jana, baada ya kupata kura 463, akimbwaga mpinzani wake wa karibu Mjumbe wa zamani wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Dk. Daniel Pallangyo, aliyepata kura (374).

Uchaguzi huo umefanyika kujaza nafasi iliyoachwa wazi na mtangulizi wake, marehemu Zelothe Stephen, aliyefariki dunia Oktoba 26, mwaka huu katika Hosptali ya Mzena iliyoko jijini Da es Saalam, alikokuwa akipatiwa matibabu ya saratani ya tumbo.

Uchaguzi huo ulisimamiwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka.

Sabaya alikuwa akichuana na wagombea wengine pia akiwamo, Solomon Kivuyo, aliyepata 59 na Edna Kivuyo aliyepata kura 10.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Sabaya, alishukuru wajumbe wa mkutano huo kwa kumchagua na wasimamizi wote wa uchaguzi kusimamia vizuri uchaguzi huo.

"Mkoa huu ulitakiwa kuwa kinara kwa chama, serikali na utulivu, maana Rais ambaye Mwenyekiti wetu anaupenda mkoa wetu kila mara yupo hapa.

"Sasa mwakani tuna uchaguzi na mwaka keshokutwa tuna uchaguzi tunaanza mradi wa kushinda uchaguzi kwa sababu tukienda kwenye uchaguzi tukiwa na makundi hatutazungumza lugha moja, lazima tukae pamoja tuchambue kero na kupatanisha watu ili tukienda uchaguzi tukashinde," alisema.






Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi wa Hanang' poleni kwa majanga

**NI** huzuni kubwa kwa wananchi wa Hanang' waliopatwa na janga ambalo hawakulitarajia lililopoteza zaidi ya watu 50 na uharibifu mkubwa wa mali, mashamba na mifugo.

Janga hilo limesababishwa na tope lililoporomoka kutoka milimani na kusambaa katika vijiji vinne na mji wa Katesh.

Kwa walioshuhudia janga hilo, wanasema lilitokea usiku wa kuamkia juzi na kusababisha wananchi kuzingirwa na maji yaliyochanganyika na tope lililosomba mawe, magogo, magari yaliyokuwa yameegeshwa na kufanya uharibifu mkubwa.

Tukio hilo likiangaliwa kupitia video fupi unaweza kudhani ni sinema ambazo zimezoeleka kuonekana katika nchi zingine, lakini limetokea nchini na kupoteza maisha ya watu wengi na kuacha majeruhi wengi.

Wananchi wa huko wanasema lilianza kwa kunyesha mvua ya kawaida, lakini baadaye ndio likatokea janga hilo la maporomoko ya tope zito lililokuwa likiteremka kwa kasi na kutokea kwa uharibu mkubwa, huku wananchi wakiachwa bila makazi na kupoteza kila kitu.

Rais Samia Suluhu Hassan, aliyekuwa nje ya nchi kuhudhuria mkutano wa COP28, amerudi nchini kuungana na Watanzania kukabili maafa hayo.

Ni janga ambalo limesababishwa na mazingira ambalo haliwezi kuzuilika wala kulaumu mtu, cha msingi ni juhudi za kulikabili na kuokoa maisha ya watu walio hatarini kwa kukosa makazi na waliopata majeraha.

Hatua za haraka zilizofanywa kupitia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini ni kujaribu kutengeneza mifereji ili maji hayo ya tope yaweze kupata njia ya kupita ili yasiendelee kuzingira makazi ya watu na kuharibu miundombinu ya barabara.

Pia wananchi ambao nyumba zao zimeharibiwa na janga hilo, wamepewa hifadhi ya muda katika shule zilizotengwa ili waweze kupata msaada wa huduma muhimu na wagonjwa wamepelekwa hospitali kwa uangalizi wa karibu.

Athari ya janga hili tunaweza kusema ni matokeo ya utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ambayo toka Agosti imekuwa ikitabiri kunyesha mvua kubwa ya El-Nino itakayosababisha maafa na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Mara nyingi utabiri kama huu hautiliwi maanani na watu kuchukulia jambo la kawaida hata hatua za kujiandaa kukabili hufanywa kwa kusuasua.

Mvua hii imeleta maafa sehemu kubwa ya nchi na watu wengi wamepoteza maisha, mashamba kusombwa na mifugo na wengine mpaka sasa nyumba zao zimezingirwa na maji na kulazimika kuondoka.

Mabadiliko ya tabianchi ni sababu kubwa ya kutokea kwa maafa kama hayo na yanasababishwa na uharibifu wa mazingira.


Pamoja na watu kukumbushwa kila mara kuwa uharibifu wa mazingira una athari kubwa kwa binadamu, lakini watu wanaendelea kuharibu kwa kukata miti ovyo.

Katika janga la Hanang' wataalamu wanasema kuna tabaka la miamba limejipanga, ambalo ni tabaka la tope liko chini, kutokana na mvua inayonyesha inawezekana maji yaliingia kwenye tabaka hilo na kukawa na mgandamizo uliosababisha tope kupanda juu ya ardhi.

Kitu kikubwa cha kujifunza kutokana na majanga yanayotokea kwa sababu ya mvua au moto ni kujiweka tayari kwa vifaa vya uokozi ili watu wasiendelee kupoteza maisha.

Tunawapa pole familia zote zilizopoteza ndugu zao kutokana na janga hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Mazingira bora ndiyo ufaulu

**HIVI** karibuni, Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), limetangaza matokeo ya mtihani wa darasa la saba wa mwaka huu, na ufaulu wa jumla ukiongezeka kwa asilimia 0.96.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, anapotoa matokeo, data za NECTA na TAMISEMI, zinaonyesha ufaulu wa kimasomo kwa daraja A, B na C vimeshuka huku Hisabati na Kiingereza ukiwa mdogo.

Ufaulu wa Kiswahili ni asilimia 87.9, Uraia na Maadili asilimia 82.12, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi asilimia 77.40, Sayansi na Teknolojia asilimia 74.08, Hisabati asilimia 48.83 na Kiingereza asilimia 34.35.

Kwa ufaulu mdogo wa masomo hayo, ni dalili kwamba kuna haja ya kuchukua hatua mbalimbali kuupandisha ili angalau ufikie ule wa Kiswahili au wa Uraia na Maadili.

Jambo la kwanza kufanyika ni kutafuta chanzo cha tatizo na kukitafutia ufumbuzi, ili tatizo lisijirudie miaka mingine ijayo, kwani kutojua lugha hiyo ni kikwazo kwao wanapoingia sekondari.

Ikumbukwe, katika shule za sekondari, Kiingereza ni lugha ya kufundishia, sio kama ilivyo katika shule za msingi, hivyo, ninadhani ipo haja kuifanya kuwa lugha ya kufundishia kuanzia shule za msingi.

Hatua hiyo inaweza kumfanya mwanafunzi kuwa na msingi wa lugha hiyo mapema badala ya kukutana nayo sekondari huku akiwa hana msingi wake, na matokeo yake anaweza kuendelea kufanya vibaya.

Pamoja na hayo, kuna haja kulipa umuhimu maalum somo la Hisabati umuhimu, kwa sababu ndio nguzo ya masomo yote mengine hasa ya Sayansi, kwani bila hisabati hakuna maisha, wahandisi wala viwanda.

Hivyo, ni vyema kuwapo walimu wa kutosha wa masomo hayo, na sio walimu tu bali wawe ni wale wanaoyamudu, ili wasaidie wanafunzi kupiga hatua kwenda mbele kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Lakini pia ipo haja ya kujiuliza kwamba, somo la Hisabati linafundishwa kwa Kiswahili ambacho ni lugha ya taifa, na ninaamini wanafunzi wanaielewa. Kwa nini bado linakuwa gumu kwa wanafunzi?

**Ufaulu wa Kiswahili ni asilimia 87.9, Uraia na Maadili asilimia 82.12, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi asilimia 77.40, Sayansi na Teknolojia asilimia 74.08, Hisabati asilimia 48.83 na Kiingereza asilimia 34.35.**

Ninadhani kuna haja pia ya kuyatazama mazingira ya kujifunza, kufundishia ambayo yanahusisha wanafunzi wao kama yanafaa kusaidia kuwafanya wafaulu au hapa.

Sio siri kwamba baadhi ya shule hazina mazingira rafiki ya kujifunza na kufundishia, hali ambayo wakati mwingine yanasababisha zisiwe na walimu wa kutosha wakiwamo wa masomo hayo.

Katika mazingira hayo, inawezekana wanafunzi wakawa wanafundishwa somo la hisabati kijuujuu na kuacha topiki nyingine, kitendo ambacho kinaweza kuchangia wafanye vibaya kwenye mtihani.

Hisabati ina topiki nyingi, ambazo ni vyema mwanafunzi azijue, kwani haujali tipoki alizojufunza, awe amefundishwa au hajafundishwa, afafanya, matokeo yake ni kushuka kwa ufaulu.

Lakini, inawezekana tatizo likawa ni wanafunzi wenyewe kutopenda somo hilo, kutokana na dhana iliojengeka kwamba hisabati ni ngumu, au walimu walionao kutolijua vizuri.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema zichukuliwe hatua mbalimbali ambazo zitachambua kiini cha tatizo katika masomo hayo na kupata ufumbuzi wake, ili ufaulu wa masomo hayo mwaka ujao, yaweze kupanda.

Hivyo, matokeo ya mwaka huu katika masomo hayo, yasaidie kuchukua hatua za kutafuta chanzo cha tatizo, kwani hata somo la Kiingereza nalo chanzo cha tatizo kinaweza kuwa kukosekana kwa walimu wanaolimudu au kwa sababu sio lugha ya kufundishia.

Ikumbukwe kuwa Tanzania haiwezi kuwa na uchumi imara na endelevu iwapo ufaulu wa somo la hisabati hautapanda, kwani ndilo msingi wa maendeleo kwenye nyanja mbalimbali za kiuchumi. Msingi mzuri wa somo hilo inatakiwa kuanzia elimu ya msingi.

## Biteko aita wadau vita dhidi ya VVU/Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewataka wadau wa mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) nchini kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kutenga fedha kukabili baa hilo badala ya kutegemea wafadhili kwa kiasi kikubwa.

Dk. Biteko alielekeza hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa mkutano maalum wa wadau wanaoshughulikia udhibiti wa VVU/UKIMWI nchini uliofanyika mjini Morogoro, ukihusisha viongozi wa serikali, watu wanaoishi na VVU na wadau wa maendeleo ikiwamo Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML).

Alisema pamoja na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali na wadau, bado UKIMWI haujadhibitiwa inavyotakiwa, hali inayoweza kusababisha maambukizi mapya kuongezeka.

Aliwataka wadau wote wanaohusika kuendelea na juhudi za utoaji afua mbalimbali zenye lengo la kutokomeza VVU/UKIMWI.

"Tanzania imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI na ninawataka TACAIDS na wadau kuhakikisha mnashirikiana kwa pamoja dhidi ya mapambano ya UKIMWI kwa kuongeza ushiriki wa wananchi pia," aliagiza.

Akichangia mada katika mkutano huo, Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa GGML, Dk. Kiva Mvungi, aliunga mkono hoja hiyo ya Dk. Biteko na kusisitiza kuwa maeneo mengine ambayo serikali inaweza kutumia na kupunguza utegemezi wa wafadhili ni kupitia kampuni kubwa zinazofanya shughuli zake nchini.

"Kwa mfano, GGML hushirikiana na TACAIDS kila mwaka kuandaa kampeni ya Kili Challenge ambayo washiriki hupanda na kuuzunguka Mlima Kilimanjaro na fedha zinazopatikana huelekezwa katika Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI pamoja na kuwezesha afua na asasi zinazojishughulisha na masuala ya VVU/UKIMWI," alisema.

Dk. Kiva alitaja mbinu nyingine ya kuondokana na utegemezi kutoka kwa wafadhili kuwa ni kushirikisha Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) ambacho kina wanachama mbalimbali zikiwamo kampuni kubwa za madini na kampuni zingine ambazo zitachangia fedha za kuendeleza mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, alisema mkutano huo ulilenga kutoa nafasi ya kushauriana kati ya serikali na wadau wake katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI.

Alisema mkutano huo ni muhimu hasa wakati huu ambao Tanzania inaelekea kufikia lengo la dunia la kumaliza UKIMWI ifikapo mwaka 2030.




Ofisa Masoko kutoka Kampuni ya Bia ya Serengeti Breweries Limited, Lusia Minja (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya 500,000/- kupitia promosheni ya Maokoto Ndani ya Kizibo, Mafuru Severine (kulia), Mkazi wa Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza kwa kuibuka mshindi kupitia bia ya Serengeti Lite, wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kikwete atunukiwa tuzo kuchochea ukuaji uchumi

**Na Dennis Fussi**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete ametunukiwa tuzo ya mafanikio ya maisha na wakurugenzi watendaji wa sekta binafsi.

Alikabidhiwa tuzo hiyo juzi jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Wakurugenzi hao, David Tarimo wakati wa hafla ya chakula cha pamoja, wakimshuruku kwa utumishi bora wa umma kutokana na mchango wake wa kuchochea kuleta maendeleo ya taifa.

Hafla hiyo ya kila mwaka ni utamaduni wa muda mrefu uliodumu kwa mwongo mmoja, ukilenga kusherehekea juhudi za serikali na sekta binafsi katika kuchangia ukuaji kiuchumi.

Kwa kutambua juhudi za ushirikiano ndio ufunguo wa mageuzi ya nchi kimaendeleo, wakurugenzi hao hutumia fursa hiyo kuwaenzi viongozi mashuhuri wa sekta ya umma ambao wameonesha uongozi wa kuigwa na kujitolea kukuza na kuwezesha maendeleo ya jumla ya sekta binafsi nchini.

Akizungumza wakati wa kumkabidhi tuzo hiyo, Tarimo alisema katika kipindi chake kama Rais Tanzania, Kikwete alikuwa kichocheo muhimu katika kuongoza juhudi za utulivu wa kisiasa ndani ya kanda na alikuwa bingwa wa kikanda kuunganisha biashara iliyoimarishwa ndani ya Afrika Mashariki.

Alisema Kikwete aliongoza diplomasia ya uchumi na kuchangia kuweka msingi imara wa kuimarisha uwekezaji nchini na ukuaji wa sekta binafsi.

Dk. Kikwete ameendelea kuwa mfuasi na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuungwa mkono kupitia msingi wake wa kubadilisha maisha kupitia uvumbuzi na ushirikiano.

"Zaidi ya hayo, katika nafasi yake kama Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kikwete anachangia katika kuwatia moyo viongozi wa kizazi kijacho wa Afrika."

Wakurugenzi watendaji hao pia walimtunuku Tuzo ya Mshirika Binafsi wa Umma kwa Mwaka 2023 Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri kwa kutambua ari na dhamira yake ya kuendeleza ukuaji wa uwekezaji.

Walisema juhudi hizo zimeongeza uwekezaji wa moja kwa moja wa fedha za kigeni kutoka dola milioni 524.4 mwaka jana hadi dola bilioni 1.05 Julai mwaka huu.

# Kituo cha afya chahitaji mil. 25/- ukarabati jengo maalum

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

KITUO cha Afya Ikwiriri, mkoani Pwani kina uhitaji wa Sh. milioni 25 kwa ajili ya jengo maalum (VIP) la kulaza wagonjwa ambalo pia litakuwa kitega uchumi cha kituo hicho.

Uamuzi wa kuwa na jengo hilo unatokana na maombi ya baadhi ya wagonjwa wakiwamo viongozi wanaopita katika barabara kuu ya Lindi-Dar es Salaam wanaofika kupata huduma kwenye kito hicho.

Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Tegemei Mtambo, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari juzi kituoni huko baada ya kupokea msaada wa viti mwendo kutoka kwa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Pwani.

Dk. Mtambo aliwaomba wadau wa ndani na nje ya Wilaya ya Rufiji kusaidia ukarabati wa jengo lililopo ili litumike kama wodi maalum ya kulaza wagonjwa ambayo itawaingizia fedha za kufanyia vitu vingine.

"Mchakato wa kupata jengo hilo ulishafanyika, tunasubiri mrejesho. Tunaomba wadau watusaidie tuweze kukarabati jengo lililopo ambalo linahitaji Sh. milioni 25.

"Likifanikiwa hilo litakuwa ni moja ya vitegauchumi vyetu, fedha tutakazopata zitatusaidia kutimiza mahitaji mengine," alisema.

Akitoa shukrani kwa UWT mkoa wa Pwani, Dk. Mtambo alisema viti mwendo hivyo vitawasaidia kubeba wagonjwa kwa kuwa awali vilivyokuwapo vilikuwa havimudu mahitaji kutokana na kuchakaa.


Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Pwani, Zaynab Vulu, alisema wametoa viti hivyo kusaidia wagonjwa ambao hawamudu kutembea wenyewe kutokana na hali zao ili wafike kwenye vyumba vya matibabu kwa urahisi.

Aliiomba serikali kuboresha kituo hicho ambacho kiko karibu na barabara ili kitoe huduma ya kulaza wagonjwa kwenye wodi maalum na kupata mapato ambayo yataingia kwenye mfuko wa halmashauri.

UWT walitoa msaada huo katika kituo hicho cha afya ikiwa ni sehemu ya kumwenzi Bibi Titi Mohamed, aliyewahi kuwa Mbunge wa Rufiji.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# ‘Watumishi shughulikieni hoja mfumo e-Mrejesho’

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi, amesema mafunzo ya kutumia mfumo wa e-Mrejesho ni ajenda na kiashiria muhimu cha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma kwa umma.

Alisema utaratibu wa kushughulikia mrejesho wa wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na serikali ni sehemu ya utekelezaji wa dhana ya ytawala bora ambayo inalenga kuzingatia na kujali matakwa na maslahi ya wengi, kuheshimu sheria, kuwa na uwazi, uwajibikaji, usikivu, haki na usawa, demokrasia, kupiga vita rushwa na kushirikisha umma katika utawala.

Pia, alisema watumishi wa umma hawana budi kusimamia ipasavyo eneo la usikivu na uwajibikaji kwa kuwapa wananchi fursa ya kuwasilikiliza ili serikali kupitia taasisi zake iweze kubaini maeneo yenye upungufu na kubadili tabia na mienendo ya utendaji miongoni mwa watumishi wa umma.

"Ninawasihi kutekeleza kwa makini mliyojifunza kwa kuwa suala la matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa umma ni utekelezaji wa maekelezo ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, anayetaka kuona inatoa huduma bora kwa umma kwa haraka na kwa ufanisi," alisema Daudi. Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi Maadili Ofisi ya Rais - Utumishi, Janet Mishinga, amesema idara yake inaendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa e-Mrejesho kwa taasisi za umma na itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji kubaini mafanikio na changamoto ili kuimarisha na kukuza uadilifu katika utumishi wa umma.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Idara ya Usimamizi Maadili imehitimisha mafunzo ya siku nne (4) kwa taasisi zilizo chini ya sekta ya afya na maji kuhusu mfumo wa kielekroni wa kutuma, kupokea na kufuatilia malalamiko, mapendekezo, maulizo na pongezi serikalini (e-Mrejesho) yaliyoanza tarehe 28 Novemba hadi tarehe 1 Disemba, 2023 katika Ukumbi Mdogo wa Chuo cha VETA Jijini Dodoma.



Mkaguzi Msaidizi kutoka Jeshi la Polisi na Mratibu wa Dawati la Jinsia vyuoni kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Gift Msowoya, akitoa elimu ya utambuzi na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mgulani wilayani Temeke jana, ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa kijinsia yanayoendelea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka yapata tuzo utayarishaji bora taarifa hesabu

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imepata tuzo ya umahiri baada ya kushika nafasi ya pili katika utayarishaji bora wa taarifa za hesabu kwa mwaka 2022/2023.

Tuzo hizo zilitolewa juzi na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) katika hafla iliyofanyika Bunju, Dar es Salaam.

DCEA ilipata tuzo hiyo kutokana na kufuata viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu hizo (IPSAS) katika kundi la wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Areta Lyimo, alisema siri ya kupata tuzo hiyo ni kazi kubwa inayofanywa na kitengo cha uhasibu kwa ushirikiano mzuri na idara nyingine ndani ya mamlaka hiyo.

Nyingine alisema uaminifu na kujitoa wakati wote kwa watumishi kwenye kitengo hicho.

"Uandaaji wa hesabu ni moja ya kazi muhimu sana katika kuiwezesha taasisi yeyote ile kufika mbali na kazi hii inahitaji uaminifu, kujituma na kujitoa. Kwahiyo nawapongeza sana kitengo chetu cha fedha na uhasibu pamoja idara nyingine ambazo wamekuwa wakishirikiana nazo," alisema Kamishina Lyimo.

"Si kwamba tu tumekuwa waaminifu katika kupambana na kudhibiti dawa za kulevya, lakini pia na kuwa waaminifu katika eneo la matumizi sahihi ya fedha za serikali na uandaaji mzuri wa hesabu kwa viwango vya kimataifa."

Alisema kwamba tuzo hiyo ina maana kubwa kwao na itawaongezea hali katika vita dhidi ya mapambano ya dawa za kulevya nchini.

Tuzo hizo za NBAA hutolewa kila mwaka kwa kushindanisha wizara, taasisi, mashirika na kampuni mbalimbali nchini.

# HKMU yaomba vyuo binafsi vipewe ruzuku

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), kimeiomba serikali itoe ruzuku kwa vyuo vikuu binafsi ili kuvijengea uwezo kuboresha miundombinu yake, kusomesha wahadhiri na mifumo yake ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Yohana Mashalla, wakati akizungumza kwenye mahafali ya 21 ya chuo hicho yaliyofanyika Mikocheni.

Kwenye mahafali hayo, wahitimu walikuwa 308 waliopata Shahada katika fani za Udaktari wa Binadamu, Ustawi wa Jamii, Uuguzi, Shahada za Uzamili na Shahada ya Heshima ya Sayansi.

Alisema kupitia mpango wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Uchumi vyuo vikuu vya serikali vimewezeshwa kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujenga kampasi mpya maeneo mbalimbali nchini.

Profesa Mashalla alisema upanuzi huo haukujumuisha vyuo vikuu vya binafsi na vingi vitaendelea kuwa na uhaba wa nafasi za kufundishia hivyo kushindwa kupunguza changamoto ya wahitimu wa elimu ya sekondari.

Profesa Mashalla alisema pamoja na changamoto mbalimbali, lakini HKMU kimeendelea kusomesha wahadhiri wake katika ngazi za Uzamili na Uzamivu ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa sasa wana wahadhiri 16 walioko masomoni na kati ya hao, tisa wanasomea Shahada za Uzamivu na saba Shahada za Uzamili na kwamba wahadhiri tisa wanasoma nchini na saba wako vyuo vya nje ya nchi.

Aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kufadhili wanataaluma wanne wa chuo hicho kupitia program ya Higher Education for Economic Transformation kwa masomo ya Uzamili na Uzamivu.

Alisema HKMU imeendelea kutathmini mahitaji yake na kuajiri wanataaluma wapya na katika mwaka wa masomo wa 2022/23 chuo kimefanikiwa kuajiri wanataaluma 16 katika ngazi mbalimbali.

Alisema chuo kinaendelea kufanya mawasiliano na balozi mbalimbali nje ya nchi kutafuta uwezekano wa kupata wataalamu wa kujitolea katika fani za afya na wenye uwezo wa kufundisha na kufanya tafiti kwenye maeneo ya kimkakati.

Profesa Mashalla alisema HKMU imefanya tathmini ya mitaala yake na kuandaa programu mpya zenye mlengo wa kutoa mafunzo yanayoendana na soko duniani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Elimu ya Afya Kairuki (KHEN), Kokushubira Kairuki, alisema sababu kubwa ya kuwekeza kwenye sekta ya afya ni ubaha mkubwa wa rasilimali watu katika sekta hiyo.

"Kutokana na maono ya KHEN ambayo ni kuboresha hali ya maisha ya binadamu sisi waanzilishi wake tuliona njia bora ya kukabili changamoto hiyo ni kuwekeza vilivyo kwenye mafunzo ya rasilimali watu kwenye sekta ya afya," alisema.

Alisema tangu chuo kianzishwe mwaka 1997, chuo kimechangia wataalamu katika sekta ya afya na ustawi wa jamii wapatao 5,413 na wengi wa wahitimu hao wako kwenye taasisi mbalimbali binafsi na za umma wakitoa huduma za afya.

"Wito wangu kwa serikali yetu ni kuendelea kuweka mazingira rafiki yatakayochagiza uanzishwaji wa vyuo vikuu vingi zaidi vinavyotoa mafunzo ya wataalamu wa sekta ya afya kukabiliana na changamoto ya maradhi kwasababu mahitaji bado ni makubwa kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani," alisema.

Aliishukuru taasisi ya Health Reach ya Canada kwa kuendelea kutoa misaada ya kifedha kwa baadhi ya wanafunzi wahitaji kwa miaka kadhaa sasa na familia ya raia wa Marekani Benjamin Christensen ambayo nayo imekuwa ikitoa misaada kama hiyo.





## Jiji Tanga laongeza kasi udhibiti wa taka

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga imeendelea kutekeleza jukumu la udhibiti taka zinazozalishwa ili zisilete madhara kwa jamii, kwa kuhakikisha magari ya uchukuzi yanaondoa taka na kuzipeleka sehemu maalumu ya kutupia.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira, Kizito Nkwabi, alisema kwenye utekelezaji huo halmashauri pia inaendelea kusajili vikundi vya ukusanyaji taka na kubainisha kuwa wakati Mwenge wa Uhuru 2023 ulipopita katika Wilaya hiyo moja ya kazi zilizofanywa ilikuwa ni uzinduzi wa gari jipya la kubeba taka la halmashauri hiyo.

Nkwabi alisema gari hilo tayari lipo mtaani likiendelea na kazi, ikiwa ni moja ya mipango ya halmashauri ya ununuzi wa magari ya kubeba taka ili kurahisisha kazi ya uondoaji wa taka katika mitaa.

Alibainisha kwamba pamoja na ununuzi wa gari hilo, halmashauri inafanya matengenezo ya vifaa na magari mengine ili kuongeza nguvu katika eneo hilo, huku ikijipanga kununua magari ya kisasa zaidi na kuachana na vifaa vilivyopitwa na wakati.

Alifafanua kuwa jiji hilo lina kata 27, ambazo kwa pamoja zinazalisha zaidi ya tani 217 za takataka kwa siku katika kaya, biashara, viwanda, na mifugo. Mbali na jiji kuongeza uwezo wake, lakini inashirikisha sekta binafsi, na tayari jambo hilo linafanyika katika kata za Nguvumali, Pongwe na Maweni.

"Tayari tunawatambua wadhibiti taka 430, kwa kutumia mfumo wa urejelezaji taka kuwa mali au kuzirudisha taka kwenye mnyororo wa thamani ili zitumike tena kwa manufaa, na sasa hakuna taka ambayo haiwezi kutumika tena," alisema Nkwabi.

Vilevile alisema kwamba ili kupata mgawanyo mzuri wa gari za kubeba taka, halmashauri imekuwa ikitoa ratiba ya magari ya kubeba taka kwa kila kata, huku akitoa rai kwa wananchi na viongozi katika ngazi husika.

"Niwaombe viongozi na jamii kwa ujumla, kuhakikisha taka zinawekwa katika vifaa vya kuhifadhia, na watoe taka kwa mujibu wa ratiba ya siku ya kupita gari, lakini wasimpe taka mtu asiye rasmi, ambaye hajaidhinishwa na halmashauri kufanya kazi hiyo, mfano unampa taka mtu halafu anaziacha mtaa wa pili, hii sio sawa," alisisitiza.

Pamoja na hayo Kizito aliwakumbusha wananchi kulipia huduma hiyo, kwa kusema "hii ni sawa na ule usemi wa 'haki huenda na wajibu', watu walipie ada ya huduma hii ambayo kwa kaya ni Sh. 2,000 kwa mwezi, huku maeneo ya biashara yakiwa na viwango vyao kwa mujibu wa ukubwa na aina ya biashara."

# Wadau wakutana kunusuru utamaduni jamii Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KUKOSEKANA kwa taasisi maalum inayowajibika moja kwa moja na uhifadhi wa urithi wa utamaduni wa jamii za Kilimanjaro unaotishia kupotea, kumewaibua wadau kutoka mikoa mbalimbali nchini, kupigania kufufuliwa kwake.

Aidha, wadau hao kupitia Taasisi ya Umataduni ya Kilimanjaro (KCF), wameanzisha mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia, vita dhidi ya mapenzi ya jinsia moja na madarasa maalum ya kupambana na mmomonyoko wa maadili kwenye koo za makabila yote yaliyoko Mkoa wa Kilimanjaro.

Akizungumza katika Manispaa ya Moshi, juzi, Mwenyekiti wa KCF, Ansi Mmasi, alisema wameamua kufanya hivyo kwa kuwa kuna viashiria vya kutotiliwa maanani utamaduni huo kwa sababu hakuna mtu au taasisi maalum inayowajibika kufanya hivyo.

Alisema mara nyingi hakuna maelezo kuhusu eneo au wamiliki wa vitu vya urithi wa kitamaduni vinavyopatikana katika maeneo ya jamii ya Kilimanjaro hali inayoleta ugumu wa kuvifahamu.

"Ni vigumu sana kujifunza, kurithi desturi au kupata muktadha wa shughuli fulani ya jamii ya Kilimanjaro na asili yake. Jamii ya watu wa Kilimanjaro wengi wamehamia sehemu nyingine za nchi na dunia, ambako wengi wa kizazi kipya wanalelewa. Bila juhudi za makusudi za kufufua, kuhifadhiana, kukuza maadili ya utamaduni na kimila, utamaduni na urithi wake mambo hayo yatakuwa hatarini kutoweka," alisema.

Kwa mujibu wa Mmasi, KCF itatumika kufundisha mila na tamaduni za Kilimanjaro, kwa kutumia viongozi wa koo. Inalenga kutoa elimu ya mmomonyoko wa maadili kwa vijana na kutoa fursa za kiuchumi, utalii kwa jamii na koo za makabila ya Kilimanjaro.

Pamoja na mambo mengine, alisema KCF inatarajia kufanya tamasha la utamaduni la Kilimanjaro, Desemba 27 na 28 mwaka huu, ambalo litaongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki.

Kwa mujibu wa Mmasy, washiriki wa tamasha hilo watapata fursa ya kutembelea vivutio vya kitalii vya utalii vilivyopo mkoani humo pamoja na mapishi ya vyakula vya asili.

"Tunategemea watu zaidi ya 1,000 wa koo mbalimbali za mkoa wa Kilimanjaro ambao wataonyesha tamaduni na za koo husika kwa lengo la kuelimisha jamii ya mkoa huu ambayo imetoka kwenye uasili wake na kuiga tamaduni za magharibi," alieleza zaidi Mmasi.

Alisema washiriki watapata fursa za kiuchumi na utalii, ambapo watatembelea Mapango ya Marangu, Mapango ya Nubi na Maporomoko ya maji ya maeneo mbalimbali mkoani Kilimanjaro.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro (CCM), Patrick Boisafi, amesema wao kama wabia wa serikali wanaona mwanga katika utashi huo, kwa kuwa utafundisha jamii na viongozi wa koo mbalimbali.

Boisafi, alisema kuwapo kwa taasisi hiyo, kutasaidia kutoa elimu ya kiuchumi na kuhamasisha jamii kutembelea vivutio vya kitalii, hasa mwezi Desemba, ambao wakazi wa Kilimanjaro huzuru mkoa huo kwa ajili ya sikukuu za mwisho wa mwaka.



Mwenyekiti wa Mtaa wa Tanesco, Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Justin Abraham (aliyesimama), akisisitiza wazazi na walezi wa shule za msingi Mirerani, Jitegemee na Endiamtu, wachangie chakula shuleni jana, kushoto ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Endiamtu, Charles Msangya na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mirerani, Tenesia Katukuru. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC aagiza pesa zinazokusanywa na halmashauri zipelekwe benki

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amezipiga marufuku halmashauri zote za wilaya na miji za mkoa huo kukusanya mapato ya serikali na kubaki na fedha mbichi bila kuipeleka benki.

Aidha amezinyooshea kidole halmashauri ambazo ukusanyaji wake wa mapato uko chini kuwa chanzo chake ni kuwapo migogoro kati ya wakurugenzi, wataalamu na wenyeviti wa halmashauri.

Sendiga alipiga marufuku hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza kwenye kikao cha kamati ya ushauri ya Mkoa (RCC). Alisema mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2023/24 kuanzia Julai mpaka Novemba wameishakusanya mapato kwa asilimia 52.

Alisema licha ya kukusanya asilimia 52 ya mapato wako vizuri, ila bado Sh. mil. 126 ziko mkononi mwa halmashauri hali inayoleta shida mkaguzi wa serikali anapopita kufanya mahesabu.

Alisema fedha ambazo bado ziko mkononi kila halmashauri wilaya ya Mbulu Sh. mil. 11, Hanang' Sh. mil. 36.3, Kiteto Sh. mil. 17, Mbulu Mjini Sh. milioni sita, Simanjiro Sh. mil. 15, Wilaya ya Babati Sh. mil. 31 na Mji wa Babati hakuna fedha iliyopo mkononi.

Aidha kuhusu hali ya ukusanyaji alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ina asilimia 69, Hanang' 63, Kiteto 51, Wilaya ya Babati 50.2, Babati Mjini asilimia 50, Mbulu Mjini 45 na Simanjiro 35.

Mkuu huyo wa mkoa alisema sababu zinazotolewa na halmashauri za kubaki na fedha mbichi kuwa ni shida ya mawasiliano au mazingira magumu ni uongo kwanini wakusanya mapato wanafika halafu washindwe kupeleka fedha benki.

Alisema halmashauri ambazo mapato yake yako chini ndio kuna migogoro ya wakurugenzi na wenyeviti au Mkurugenzi na mtunza hazina.

Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA, Iddy Msuya, alisema miji yote inayosimamiwa na BAWASA upatikanaji wa maji ni asilimia 80 kutoka asilimia 69 mwaka jana huku mradi uliosaidia kuongeza upatikanaji wa maji ni wa Dareda-Singu mpaka Bagara ambao kwa sasa unatoa maji matamu.

Mkurugenzi huyo alisema upatikanaji wa maji katika eneo hilo ni saa 16 na wana vyanzo 30 vya maji.

Naye Kaimu Meneja wa RUWASA mkoani Manyara, Amina Mwanja, alisema wao wanahudumia vijiji 388 na wamefikia asilimia 75 za upatikanaji wa maji. Miradi ya kimkakati wanayotekeleza kuwa ni Bassout vijiji saba, Madunga vijiji saba, Mogitu vijiji saba, mradi wa Mbulu utanufaisha watu zaidi ya 100,000.





# Wakazi Busangi walia uhaba maji

Na Shaban Njia, KAHAMA

WAKAZI 14,894 wa Kata ya Busangi Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wanalazimika kutumia maji yasiyo safi na salama katika visima walivyovichimba jirani na nyumba zao kutokana na gharama kuwa kubwa kwa ndoo moja ya lita 20 kuuzwa kwa Sh.500.

Inaelezwa kuwa matumizi ya maji hayo yamekuwa yakisababisha kuibuka kwa magonjwa mbalimbali ikiwamo watoto kuhala damu, typhoid pamoja na UTI huku majisafi yakipatikana umbali wa kilometa 10 katika kata za jirani.

Mkazi wa kata hiyo, Selina Samweli, alisema kwa sasa wanalazimika kununua maji ndoo moja ya lita 20 kwa Sh. 500 na wale wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama hizo wanalazimika kutumia maji hayo ambayo si salama kwa afya zetu.

"Kuna muda tunaamua kufuata maji safi katika kata jirani za Nyaga na Masabi lakini tunapigwa na waume zetu pale tunapochelewa kurejea nyumbani, wanafunzi hasa wa kike wanakosa masomo yao kwasababu ya kuambanata na wazazi kutafuta maji tunaomba mradi unaotekelezwa ukamilike kwa wakati," alisema Selina.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Busangi, Msafiri Yohana, alisema, shule hiyo inajumla ya wanafunzi 1,251 na wanaongoza kwa utoro shuleni ni wanafunzi wa kike kulinganisha na wa kiume kwa sababu wanashirikiana na wazazi wao kutafuta huduma ya maji.

Kaimu Meneja wa RUWASA-Kahama, Mhandisi Paschal Mnyeti, alisema katika kata hiyo unajengwa Mradi wa Maji na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa gharama ya Sh. bilioni 5.310 na unatarajia kukamilika ifikapo Julai 2023.

Akitoa taarifa ya mradi huo wakati wa ziara ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mnyeti alisema, ujenzi wake ulianza Julai 2020 na unakamilika mwishoni mwa mwezi huu kwa awamu ya kwanza na utahudumia wakazi 11,630 wa vijiji vya Busangi, Nyamigege na Ntundu, awamu ya pili vijiji vya Gulla, Ntobo, Masabi na makao makuu ya Halmashauri ya Msalala.

Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddi Kassimu alisema, jimbo hilo limepokea Sh.bilioni 12 za upelekaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi na sasa ujenzi unaendelea katika maeneo ya Mwazimba, Mwashigini, Buyange, Ilogi, Bulyanhulu na Kata ya Ikinda hivyo kila mwananchi atakunywa majisafi..




Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Dk. Vincent Mashinji, akipanda mti kwenye hafla ambayo Kampuni ya Bayport ilitoa msaada wa miche ya miti ya matunda 500 kwa Shule ya Msingi Muungano na Sekondari ya Mapinduzi za Serengeti, mkoani Mara, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha Watanzania kutunza mazingira kwa kupanda miti 1,000,000 nchini kote mwishoni mwa wiki. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Bayport, Bwana Nderingo Materu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waganga zaidi ya 600 wafungiwa kutoa huduma za tiba za asili

Na Rose Jacob, UKEREWE

ZAIDI ya waganga wa kienyeji 600 wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, wamefungiwa kutoa huduma ya tiba za asili kwa muda usiojulikana mpaka watakapopata mafunzo na kufikia kiwango cha kuwa wataalamu wa tiba hiyo kwa mujibu wa sheria.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mganga Mkuu wa Wilaya ya UKerewe, Dk. Charles Mkombe, wakati wa mahafali ya mafunzo ya waganga wa tiba za asili, wauza dawa, wakunga na tiba mbadala katika halmashauri hiyo.

"Hakuna Mganga yeyote ambaye atatoa huduma bila kukizi vigezo, wilaya hii ina waganga wa jadi 623, waliyopata mafunzo ni 15, lakini 608 wanapigapiga chenga wakiwasikiliza matapeli, sasa watambue tunaanza msako na hawatapata leseni," alisema Mkombe.

Mhitimu wa mafunzo hayo ya siku saba yanayotolewa na Chuo cha Mwanza Polytechnic Institute, Jumanne Mfaume, alisema uwepo wa gharama kubwa za upimaji na usajili wa dawa katika maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali zinasababisha wataalamu wa tiba asilia kushindwa kumudu gharama hizo.

Naye Mkurugenzi wa Chuo cha Mwanza Polytechnic Institute, Dk. Jelly Ngussa, alisema utafiti unaonyesha asilimia 60 ya Watanzania wanatumia tiba asilia zinazotolewa na waganga wa jadi hivyo wanapaswa kupata ujuzi ili kutoa matibabu yaliyo na tija.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Ukerewe, Joshua Manumbu, aliishukuru serikali kwa kusaini mkataba na nchi ya India kwa ajili ya kujenga hospitali kubwa ya tiba asilia kwani itakuwa msaada kwa wataalamu wa tiba asilia nchini.

"Sasa mtakuwa mabalozi wazuri kwa waganga wengine, tuhakikishe tunafanya kazi kwa weledi na kufuata sheria na taratibu za nchi tushirikiane kudhibiti masuala ya ramli chonganishi, mgonjwa anaumwa TB hadi anakohoa damu wewe unaendelea kumpatia dawa za kienyeji nina imani nyinyi hamtokwenda kufanya hivyo," alisema Manumbu.

# TRA Kahama yakusanya bil. 6.5/- robo ya kwanza ya mwaka

Na Neema Sawaka, KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa kikodi Kahama, imekusanya Sh. bilioni 6.59 kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuanzia Julai hadi Novemba sawa na ufanisi wa asilimia 125.

Kaimu Meneja wa TRA Kahama, Wisaka Kamwamu, alibainisha hayo juzi katika kilele cha maadhimisho ya siku ya shukrani kwa mlipakodi na kutaja biashara ya magendo kuwa kikwazo katika ukusanyaji kodi mkoani hapa.

"Shughuli ya ukusanyaji wa kodi ni endelevu inahitaji uimara siku hadi siku na wafanyabiashara wanapouza watoe risiti na wateja wadai risiti kwani usipodai risiti unarudisha nyuma jitihada za serikali kufikia malengo yake," alisema Kamwamu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Fedha kutoka TRA Makao Makuu, Anna Mdeme, aliwasihi wafanyabiashara kutoficha taarifa zao ili kuwezesha ukusanyaji mapato, kwa kuwa huduma bora zenye uwajibikaji ndiyo msingi bora wa kulipa kodi na mamlaka inaendelea kutoa elimu zaidi ili kuleta uwajibikaji kwa walipakodi.

"Matumizi sahihi ya mashine za EFD ndio msingi wa kupata takwimu sahihi za biashara na kuwezesha ukadiriaji na ukusanyaji wa kodi sahihi unaopelekea kupunguza na kuondoa malalamiko ya ukadiriaji wa kodi kwa wateja," alisema Mdeme.

Alisema kuanzia Julai hadi Septemba ambayo ni robo ya kwanza ya mwaka wa fedha makusanyo yaliyofanyika kitaifa ni Sh.trilioni 6.58 sawa na ufanisi asilimia 97.53 ya makusanyo hayo ni ongezeko kubwa la asilimia 11.05 huku mwaka uliopita walikuwa na ongezeko la asilimia 8 pekee.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni alikemea mbinu inayotumiwa na baadhi ya wafanyabiashara kwa wateja wao kwa kuwapa uchaguzi kuwa wakitaka risiti ni Sh.120,000 na usipochukua risiti ni Sh.80,000 ikiwa na lengo la kuwafanya wateja wasidai risiti ili wakwepe ulipaji wa kodi kwa njia hiyo.

"Kauli mbiu ni 'Kodi yetu maendeleo yetu tuwajibike' ili kuwa na kumbukumbu sahihi za biashara yako lazima ujue kodi inayotozwa hivyo utunze kumbukumbu na hapo utalipa vizuri kuliko wasiotunza kumbukumbu," alisema Mhita.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Wilaya ya Kahama, Charles Machali, alisema kutunukiwa vyeti wafanyabiashara na kuongezeka mapato ni jitihada zilizofanywa na wao katika kuhamasisha kuwa kodi ni maendeleo na ndiyo maana kila kukicha biashara inaanzishwa.



Ukurasa 14

Ajira Portal mlango wa kupata kazi za utumishi wa umma





Ukurasa 12

Ndoto za Mwenyekiti Joyce Shebe kuipaisha TAMWA kimaendeleo

Nipashe
TESA
Jumanne Desemba 5, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

TEKNOLOJIA

NA FRANK MONYO

# Bajaji ya umeme ilivyo nyenzo nafuu kwa kijana msafirishaji

KILA kukicha, siku inaanza na mafanikio ya kukua na kusambaa teknolojia, kunakoambatana na mbinu na mambo mapya ya kurahisisha utendaji kazi na kupunguza gharama za maisha.

Katika hilo, kampuni ya TRí ya Dar es Salaam, haiko nyuma kuleta mabadiliko kiteknolojia, ikiibuka na bajaji ya umeme, inayoelezwa kuwa ni hatua ya ukombozi kwa vijana na wamiliki wa chombo hicho.

Bajaji ina sifa ya kuwa na kasi, lakini kupenya na kuzifikia kona nyingi, ambazo gari kubwa haliwezi. TRí inaandika historia, kuunda bajaji za umeme, zenye betri mbili na chaja inayozijaza nguvu kwa kasi kuanzia saa 2:00 hadi 6:30 kila zinapopungua chaji.




Mercy Kitomari, Ofisa Uhusiano wa Biashara na Uhusiano Serikalini wa TRi katika mahojiano na Nipashe, anaeleza kuwa kampuni hiyo imekuja na ubunifu wa bajaji za umeme zenye matumizi nafuu ikilinganishwa na za mafuta.

Nia yao ni kubadilisha maisha ya vijana na kuipa thamani biashara hiyo, kwa kuwapunguzia gharama vijana 'wanaohaso' kutafuta maisha kwenye usafirishaji, anasema Mercy.

Anaeleza bajaji hiyo ni mkombozi wa uchumi wa madereva hao ukiwaondoa kwenye kutumia gharama kubwa ya mafuta pamoja na matengenezo ya dharura.

"Bajaji hii inatumia betri mbili, na kujaza betri moja unatumia umeme wa Shilingi 3,000 kwa kutumia umeme wa kawaida wa nyumbani na ikijaa ina uwezo wa kutembea kilometa 100 mathalani kutoka Ubungo hadi Chalinze.

Hilo ni mosi, mbili ni suluhisho la usafi wa mazingira, hurahisisha maisha ya madereva na wamiliki pamoja na kumpa utulivu abiria awapo safarini ukilinganisha na za mafuta ambazo zina kelele na nyingine kutoa moshi," anasema Mercy.

Mpaka sasa kuna bajaji 20 ambazo zipo mtaani, na kwamba amezikaribisha taasisi mbalimbali zinazotumia usafiri huo katika shughuli zao kugeukia za umeme kwani uendeshaji wake ni nafuu na hulinda mazingira, anaongeza.

Ofisa Uhusiano anaeleza kuwa pale mteja anaponunua bajaji hizo wanampa ofa ya mwaka mmoja kufanyiwa matengenezo na usimamizi na TRi na akikumbusha kwamba gharama za bajaji za umeme na za mafuta zinaendana sokoni.

"Bajaji zetu na za mafuta zinalingana bei sokoni, zote zinauzwa Shilingi milioni 8.6 tunampatia mteja nyaraka zote muhimu, betri mbili na chaji yake," anasema Mercy.

Kampuni hiyo kwa sasa inafanya mazungumzo kwa ajili ya ushirikiano na halmashauri au taasisi nyingine ili kuzitoa kwa mikopo na kuwawezesha vijana kumiliki bajaji hizo, anaeleza.

"Kama unasema unataka kumwezesha mwanamke au kijana, kwa kumpatia bajaji ya mkopo, basi unapaswa kumwondolea na gharama ya mafuta na matengenezo kwa kumpatia bajaji zetu za umeme, hiyo itamsaidia sana kujikimu na kuongeza thamani ya kazi anayofanya kwani atapata faida kubwa," anasema Mercy.

"Sisi kwetu tunaona dereva wa bajaji ni kama mfanyabiashara, hivyo tunampa unafuu wa kuendesha biashara yake ili ajiongezee kipato na kubadilisha maisha yake, kwa hiyo katika uendeshaji wa bajaji ya umeme na wa mafuta, umeme ni nafuu sana," anasema

Mercy, anasema ugunduzi wa bajaji hiyo unampunguzia dereva mzigo na kuongeza:

"Dereva wa bajaji ya mafuta akiamka anawaza kuweka mafuta ya kuanzia kazi, lakini ya umeme ukiamka unaichaji kwa gharama ndogo ya Shilingi 3,000 na kuokoa zaidi ya 40,000."

## UZALISHAJI

Mercy anasema bajaji hizo zinatengenezwa kwa ushirikiano na wahandisi kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar Es Salaam (DIT) kwa ushirikiano na TRi.

"DIT ni suluhisho kwetu, kwani unapoanzisha bidhaa mpya sokoni, hasa kwenye ufundi, unahitaji kuwa vizuri kuanzia mwanzo, tunafanya vitu vitatu na DIT."

Cha kwanza kuziunda kwa kutumia mafundi wao, tunabadilishana ujuzi, kwa maana wanafunzi wa DIT watajifunza kupitia bajaji zetu, kingine tunafanya utafiti wa kibiashara," anasema Mercy.

Anaongeza kuwa ujio wa bajaji hizo ni fursa mpya kwa mafundi kwani matengenezo yake ni tofauti na za mafuta, akiwahimiza vijana na mafundi kujifunza kutengeneza bajaji za umeme kupitia DIT ili kujiongezea kipato.

Dereva wa bajaji, kutoka katika kituo cha Mwenge Mpakani Dar es Salaam, anapozungumzia biashara yao, anasema ni mkombozi.

Jerome Kashangaki, ni dereva wa bajaji namba MC 789 BCS, anayesema kupanda bei za mafuta ni mwiba katika kazi zao sambamba na mizozo kutoka kwa wamiliki wa bajaji, hasa usipowasilisha mapato ya siku au wiki.

"Bajaji ni nyingi mjini, biashara imekuwa ngumu mno tunavurugwa na kupanda bei za mafuta. Kwa mfano, kutoka Mpakani Mwenge hadi Mbezi ukimtajia abiria nauli ya 3,000 hakuelewi, hataki kusikia wakati mafuta bei imepanda," anasema.

Anaongeza:"Hapo bado jioni mmiliki anataka hela yake, ukipiga hesabu mfukoni hakuna kitu biashara hii ni ngumu sana tutafanyaje na ajira hakuna, tunakomaa tu."

ELIMU
NA MWANDISHI
WETU

# Ndoto za Mwenyekiti Joyce Shebe kuipaisha TAMWA kimaendeleo

- Uwekezaji ardhi na majengo ya vitega uchumi Dar na Zanzibar
- Nyumba za hifadhi pia vituo vya taarifa, maarifa kujuza wanawake

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake TAMWA, kimetimiza miaka 36, kikisherehekea mafanikio na mchango wake kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto na ushiriki wao kukuza uchumi, uongozi na siasa, kazi ikifanyika kupitia vyombo vya habari.

Chama kinamkaribisha Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa mgeni rasmi katika 'jambo la TAMWA' linalofanyika Dar es Salaam hivi karibuni. Mwenyekiti wa TAMWA Joyce Shebe, ana mengi kwa wanachama na kwa Rais, katika hotuba ya makaribisho, anasema, maono ya chama ni kuwa na Tanzania inayoheshimu haki za binadamu kwa mrengo wa usawa wa jinsia kwa kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto, kupitia vyombo vya habari.

Anasema kwa miongo minne sasa inafanya uchechemuzi wenye kuongeza ushawishi kuhusu elimu ya usawa wa jinsia, kupinga mila na desturi kandamizi, ukatili wa jinsia, kushawishi na kuchochea ushiriki wa wanawake katika uongozi, siasa, uchumi na ushawishi wa kutungwa kwa sheria, sera na kanuni zinazohusu usawa.

Anaitaja kaulimbiu ya maadhimisho ya miaka 36 ya 'uongozi bora na mchango wa wanawake ni chachu kuelekea Tanzania yenye maendeleo endelevu,' akisema inawatafakarisha mchango wa wanawake katika uchumi, demokrasia, utawala bora, kupinga na kuepusha ukatili lakini kuzitambua na kuzitumia fursa mbalimbali na namna vyombo vya habari vinavyowaandika na kutangaza mchango wao.

Joyce anamweleza Rais na wasimamizi wa masuala ya habari kuwa yanahitajika mabadiliko tena iko haja ya kuwataka watumiaji wa vyombo vya habari wa mitandaoni kuheshimu utu na haki za binadamu na kuhimiza ushirikiano na kuthaminiana baina ya wanajamii, sehemu za kazi, wana familia na kwenye majukwaa ya wazi kutambua na kuepusha viashiria vya ukatili wa kijinsia mitandaoni.



Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, katika harakati za kutetea uhuru wa habari.

> "Wengi ni mashahidi sasa taarifa nyingi za changamoto za wanawake zinaandikwa, zinazungumzwa na zinatangazwa na zinatatuliwa...

### MAFANIKIO YA TAMWA

Mwenyekiti Joyce, anaainisha mchango na mafanikio ya TAMWA kwa miaka 36 kuwa ni mengi kama ongezeko la sauti za wanawake, wasichana, watoto na wenye mahitaji maalum katika maudhui ya vyombo vya habari, mambo ambayo hayakupewa uzito kabla ya ujio wa shirika hilo,1987.

"Wengi ni mashahidi sasa taarifa nyingi za changamoto za wanawake zinaandikwa, zinazungumzwa na zinatangazwa na zinatatuliwa tena jamii imeshawishika kupaza sauti kupitia vyombo vya habari." Anasema Joyce.

Anaongeza kuwa TAMWA imekuwa kinara kudai na kushirikiana na mashirika watetezi wa haki za binadamu, kupaaza sauti za wanawake na watoto mfano kudai sheria inayotoa adhabu kwa wabakaji na kuufanya ukeketaji kuwa kosa la jinai ndiyo Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998, ambayo inaeendelea kufanyiwa marekebisho.

"Pia tumechangia kufikia mabadiliko ya Sheria ya Ardhi ili wanawake wapate haki ya kumiliki ardhi kukawa na kipengele kinachotamka kuwa kama walivyo wanaume, wanawake wana haki kisheria ya kumiliki na kutumia ardhi kwa maendeleo na nyingine zilizogusa maslahi ya wanawake, wasichana na watoto. Kwa hili tunajivunia kwani japokuwa bado tunapambana na vita ya kuzuia ukatili dhidi yao, serikali na mihimili yake inaendelea kujali na kurekebisha ama kutunga sera na sheria dhidi ya ukatili wa jinsia."

Aidha, anazungumzia rushwa ya ngono, akisema kwa muda mrefu kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) chama kikiongozwa na kampeni Vunja Ukimya Rushwa ya Ngono Inaua' kwa kiwango kikubwa imeweka mazingira rafiki kwa wanawake na wasichana kuanzia shuleni, vyuoni, sehemu za kazi na kwenye siasa kwani wengi wamejitokeza kutoa taarifa za udhalilishaji wanaokumbana nao, baadhi ya waliopatikana na hatia wameadhibiwa.

"Tatizo la rushwa ya ngono ni kubwa linaloibua mijadala yenye hisia tofauti lakini ukweli unabaki kuwa limekuwa kikwazo kwa wanawake na wasichana wengi kushindwa kufikia ndoto zao kwa wakati au wengine kuzipoteza. Katika hili, tumejikita kuhakikisha jamii inaelewa madhara yake, huku tukiangalia tasnia ya habari, ili matokeo yake yawe ni uandishi wa maudhui yanayowezesha jamii kujua ukubwa na umuhimu wa kupambana na rushwa. Itoshe kusema kuwa jarida letu la 'Sauti ya Siti' linalozinduliwa leo limesheheni shuhuda za wanahabari waliokutana na rshwa hiyo."

Anaongeza kuwa, rushwa ya ngono ni tofauti na ile ya pesa hivyo ni vyema vipengele vya marekebisho ya sheria vikasimama kumlinda mwathirika ambaye mara zote anakuwa ni mnyonge mno mbele ya mwombaji wa rushwa.

Anataja uchechemuzi wa ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi, kwa imani kuwa mwanamke ni kiongozi bora na hivyo kuwahamasisha wanawake kushiriki katika shughuli za uchumi na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kushiriki siasa kuanzia ngazi ya shina hadi taifa.

Anasema: "Nichukue fursa hii kuwahamasisha wanawake mijini na vijijini kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa 2025. Sisi wanahabari wanawake tutaendelea kuunga mkono jitihada na harakati zao na kuhakikisha tunatumia kalamu na vipaza sauti kuelimisha jamii na vyama vya siasa umuhimu wa kutoa fursa sawa na dhana ya ushirikishwaji wa jinsi zote katika siasa hasa kwenye chaguzi na teuzi mbalimbali."


Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye maadhimisho. **PICHA: TAMWA**

Kusomesha na kukuza maarifa ya wanataaluma, ni jukumu la kujivunia analotaja Joyce, akisema: "Sisi tumevaa viatu vya mama, jukumu la malezi na maadili katika jamii ni kipaumbele muhimu, tumekuwa tukiwajengea uwezo wanahabari katika kukuza weledi, kujiendeleza na kujinoa kitaaluma ili kuboresha utendaji na kuleta suluhu ya changamoto mbalimbali zinazohusu usawa wa jinsia, kukuza mila na desturi chanya na kukemea zile kandamizi kama ukeketaji, ndoa utotoni na upendeleo kwa watoto wa kiume".

Joyce anaeleza utetezi wa haki za wanawake, wasichana, watoto na wenye mahitaji maalumu kuwa ni jambo TAMWA inalojivunia pia, akisema chama kimekuwa mstari wa mbele kuibua na kupaza sauti kuhusu ukatili wa namna mbalimbali, mfano mauaji ya albino, wanawake wazee mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Tabora na Rukwa baada ya hapo hatua zimechukuliwa na tatizo linaendelea kudhibitiwa.

"Nichukue fursa hii kukushukuru Rais Samia kwa kuruhusu Tanzania kuwa ya kwanza kuanzisha vituo jumuishi vya kusikiliza masuala ya familia ikiwamo ndoa, talaka, mirathi, malezi na matunzo katika Mahakama Jumuishi zilizoko Temeke na Kinondoni Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza na Arusha. Jambo hili linaleta unafuu mkubwa kwa wanawake, wasichana na watoto wenye uhitaji."

Aidha, anamshukuru Rais Samia kwa uongozi wa kuruhusu watu kuzungumza, kujadili na kutoa hoja, pamoja na kuja na miongozo na mabadiliko ya sheria yatakayoleta ustawi. Katika mapendendekezo mbalimbali ya mabadiliko ya sheria sera na kanuni na tukisisitiza kuwa TAMWA inashauri sheria zijumuishe mtazamo wa kijinsia na kupendekeza kuwa unyanyasaji wa kijinsia kwa waandishi wa habari wanawake liingizwe katika mijadala ya masuala ya usalama na ulinzi wa waandishi wa habari, hivyo lilichukuliwa na linafanyiwa kazi, hiyo ikionyesha jitihada za serikali kutengeneza mazingira rafiki kwa wanahabari wanawake.


Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe.

Pamoja na hayo, Joyce anasema TAMWA imekuwa ikipanga mipango kazi ya kiutendaji inayoendana na mahitaji ya jamii kwa wakati, kwa mfano katika mpango kazi wake wa 2021-2025 mbali na maeneo ya kimkakati waliyoyafanyia kazi kwa muda mrefu -kupinga ukatili wa kijinsia, kushawishi na kuongeza maudhui ya usawa wa jinsia katika vyombo vya habari na mtandaoni, sasa chama kimeongeza eneo la matumizi bora ya teknolojia kwa wanawake na mabadiliko ya tabianchi kama mambo muhimu ambayo wanawake sio tu kwamba wanaathiriwa na changamoto zinazotokana nayo ila pia kuna fursa nyingi ambazo endapo watapata taarifa sahihi watafaidika na kuwajibika.

### KUINUA TAMWA

Joyce anasema ili TAMWA iendelee kustawi na kutoa huduma zake katika tasnia ya habari, wanawake, wasichana na watoto imewekeza na kumiliki ardhi ambako ndiko ziliko ofisi za chama Sinza jijini Dar es Salaam, akisema shirika linaendelea kutimiza makusudi ya kujenga vituo vya maarifa (Resource Centres) huko Sinza, Dar es Salaam, Tunguu Zanzibar na kule Msufini mkoani Pwani ambapo kuna hekari 96, ambazo pia chama kina mpango wa kujenga kituo cha maarifa kitachowezesha wanaweke kujifunza mambo mbalimbali yakiwamo yanayohusu uongozi.

> "Sisi tumevaa viatu vya mama, jukumu la malezi katika jamii ni kipaumbele muhimu, tumekuwa tukiwajengea uwezo wanahabari katika kukuza weledi...

Anaushukuru mkono wa serikali kufanikisha nia ya kuwekeza kwenye kilimo akisema: "Kwa msaada wa Wizara ya Kilimo, na hapa tumshukuru sana Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ambaye tulimweleza kwamba TAMWA tuna shamba na tungependa kulima kibiashara hivyo tulimwomba tupimiwe udongo ili tuweze kujua nini kinastawi na mbolea ipi tutatumia. Waziri alilipokea na wataalamu wa Wizara wameshaupima udongo. Nia yetu ni kupunguza utegemezi kwa wafadhili ambao hata hivyo wanaendelea kupungua kila kukicha."

### MKONO WA SERIKALI

Mwenyekiti wa TAMWA anaamini kuwa serikali ni mama ambaye kila mmoja anamwamini na kumtegemea akisema: "Ombi letu kwako mheshimiwa ni kuendelea kutuunga mkono katika juhudi zetu za kuwa na Tanzania inayoheshimu haki za binadamu kwa mtazamo wa kijinsia. Pia tunaomba serikali itusaidie wataalamu na miundombinu ya umwagiliaji katika shamba letu Msufini, Kibaha Vijijini Mkoa wa Pwani.

"Aidha, ikikupendeze pia mheshimiwa Rais kutuwezesha kuweka msingi na kujenga jengo letu la maarifa la ghorofa tano Sinza Mori na kuendeleza jengo lingine kule Tunguu Zanzibar ambapo kote tuna mpango wa kuwa na kumbi za mikutano na nyumba salama kwa ajili ya wanawake, wasichana na watoto wanaotukimbilia wanapokumbana na vitendo vya ukatili."

Kadhalika, kwa niaba ya TAMWA Mwenyekiti anamwomba Rais kupitia washauri wake wa mabadiliko ya tabianchi, kuja na mpango wa elimu kwa wanahabari kuhusu mabadiliko ya tabianchi ili waweze kuongeza tija ya uelewa wa masuala haya kwa wananchi, akimalizia kwa kuahidi kuwa wana TAMWA wataendelea kutumia taaluma kuunga mkono kazi nzuri anazofanya za kuendeleza jamii inayoheshimu haki za watu wote, hususan wanawake na watoto, wenye mahitaji maalum kwa maslahi ya Tanzania.

ELIMU

NA MOSHI LUSONZO

# Ajira Portal mlango wa kupata kazi za utumishi wa umma



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Lynn Chawala, akisalimiana na Naibu Waziri Utumishi, Ridhiwani Kikwete. **PICHA: MWANDISHI WETU**

KATIKA mapinduzi ya kiteknolojia, karibu mambo yote hufanywa mtandaoni. Kadhalika, vijana wanaoomba kazi serikalini, husaka ajira kielektroniki.

Badala ya kuandaa barua kwenye makaratasi na kuzipitishia posta, sasa hutumia muda mfupi kuwasilisha maombi ya ajira wakiwa popote wakitumia simu janja.

Ni mabadiliko yanayoletwa na Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira inayoandaa 'Ajira Portal'. Kutokana na ukweli kuwa vijana wengi humaliza masomo kila mwaka, kadhalika idadi kubwa ingependa kufahamu namna ya kupata kazi serikalini.

Ili kujitafakari na kuelewa walikwama wapi kwenye juhudi za kufikia nafasi za utumishi wa umma, Mkuu wa Mawasiliano Sekretarieti ya Ajira, Lynn Chawala, anajibu hoja za baadhi ya waombaji kazi, katika mahojiano na Nipashe yanayofanyika Dar es Salaam hivi karibuni.

Anaanza kueleza kuwa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ndicho chombo kinachohusika na kupata watumishi au nguvukazi inayotumika katika ofisi mbalimbali za umma na serikali.

**SWALI: Ni njia gani mnazotumia kuepuka malalamiko kutokana na usaili unaokuwa na idadi kubwa ya waombaji kuliko nafasi zilizopo?**

**JIBU:** Sekretarieti huendesha usaili wa aina tatu, kwa mujibu wa kanuni ukiwamo wa kuandika, wa vitendo na mahojiano na kote huko hufanyika mchujo ili kuwapata waombaji wenye sifa kulingana na nafazi inayohusika.

**SWALI: Kwa nini mfumo wenu umezuia watu waliosoma shahada ya kwanza kuomba kazi ya cheti ikiwa wana sifa na hajapata kazi?**

**JIBU:** Jambo hili ni la kisera zikitaka ushindani ufanyike kwa haki na usawa. Mfumo wa "Ajira Portal" unawawezesha watafuta kazi serikalini kuingiza taarifa binafsi zikiwamo za kitaaluma. Matangazo ya ajira yanapotoka huweka bayana kiwango cha elimu kinachohitajika ili haki itendeke kwa wasailiwa wote.

**SWALI: Vipi nafasi ya watu wanaoishi na ulemavu katika mchakato wa ajira, ukoje?**

**JIBU:**Sekretarieti hutangaza ajira kwa wote bila kujali jinsi, hali za kijamii au changamoto alizonazo mwombaji. Ajira katika utumishi wa umma hupatikana kwa kushindanisha waombaji wenye sifa. Hata hivyo, mfumo wa Ajira Portal unawawezesha wenye mahitaji maalum kuingiza taarifa za ulemavu wao ili kuhudumiwa wakati wa mchakato.

**SWALI: Mmekuwa na kawaida ya kukagua vyeti vya kitaaluma siku za usaili, je, kwa watu waliovipoteza inakuwaje?**

**JIBU:** Lengo ni kuhakikisha msailiwa ana cheti halisi na ndiye anayefanya usaili huo. Wapo baadhi ya waomba kazi ambao vyeti vya taaluma vimepotea, wanapaswa kutoa taarifa za upotevu polisi, kutoa tangazo kwenye gazeti, kwenda kwenye taasisi walikosemea au Baraza la Mitihani la Taifa kwa utaratibu mwingine.

**SWALI: Mnazingatia madaraja ya ufaulu katika elimu ya vyuo vikuu kwa waombaji?**

**JIBU:** Zipo baadhi ya kada ambazo masharti yake ni pamoja na kuwa na kiwango fulani cha ufaulu, lakini nyingine hazina masharti kinachoangaliwa ni ufaulu na sifa zilizoainishwa katika tangazo, kwa hiyo sio wakati wote.

**SWALI: Muundo wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ukoje?**

**JIBU:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira inaongozwa na mwenyekiti akisaidiwa na wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi saba, katibu ndiye mtendaji mkuu wa taasisi.

Dhima ya sekretarieti ni kuendesha mchakato wa ajira kwa kutumia mbinu za kisasa na kwa kuzingatia kanuni za sifa, usawa, uwazi pamoja na kutoa ushauri kwa waajiri kuhusu masuala ya ajira.

**SWALI: Majukumu ya chombo hiki muhimu ndani ya serikali ni yapi?**

**JIBU:** Jukumu la msingi la ofisi hii ni kuwezesha mchakato wa ajira katika utumishi wa umma. Lakini pia kuna majukumu mahsusi ya kisheria ambayo ni pamoja na kutafuta na kuwaajiri wataalamu wenye ujuzi maalum na kuandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa.

Kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika utumishi wa umma, kuhusisha wataalamu maalum kwa ajili ya kufanya usaili kulingana na mahitaji na kutoa ushauri kwa waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na ajira.

**SWALI: Nini lengo la kuanzishwa kwake?**

**JIBU:** Kuna mambo mengi yaliyosababisha serikali kuanzisha chombo hiki lakini muhimu zaidi ni kuendesha mchakato wa ajira kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni pamoja na taratibu kwa kushirikiana na wizara, idara, wakala wa serikali, taasisi za umma na mamlaka za serikali za mitaa.

**SWALI: Mchakato wa ajira katika utumishi wa umma ukoje?**

**JIBU:** Ni vyema watu wakatambua kuwa Sekretarieti imekuwa ikiendesha mchakato wa ajira kwa uwazi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Sekretarieti hupokea kibali kutoka kwa waajiri ambacho kimeainisha idadi ya nafasi na kada anazozitaka kwa mujibu wa sifa na vigezo vya muundo.

Baada ya hatua hiyo, huandaa tangazo kwa kushirikiana na mwajiri ambalo linaainisha kwa uwazi mwajiri ni nani, nafasi zinazotangazwa, kada inayotakiwa, sifa za anayetakiwa na vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa.

Maombi yakitumwa huchambua ya kila mwombaji ili kuandaa orodha fupi miongoni mwa maombi yote. Kisha huandaa tangazo la kuwaita waombaji waliokidhi vigezo kwenye usaili na kuhakikisha tangazo linawekwa kwenye tovuti ya sekretarieti kwa siku saba na vyombo vingine vya mawasiliano.

Tukimaliza hapo tunawashindanisha wasailiwa kulingana na mahitaji ya nafasi iliyotangazwa.Wasailiwa hupitia usaili wa kuandika ambapo hupewa maswali na kuyajibu kwa kuandika kutegemeana na kada, pia wengine watatakiwa kufanya usaili wa vitendo na kumalizia na mahojiano kulingana na kada husika.

Wasailiwa waliofaulu huandaliwa barua za kupangiwa vituo vya kazi. Majina yao na sehemu wanazopangiwa hutolewa kupitia tangazo.

**SWALI: Mfumo gani hutumika kupata kazi serikalini, unaweza kueleza ili watu wenye sifa wautumie?**

**JIBU:** Mfumo unaotumika kutuma au kuomba kazi unaitwa Ajira Portal, ambao maombi huwasilishwa kielektroniki mtandaoni na umebuniwa na kujengwa na wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa sekretarieti ukiwa na lengo la kurahisisha mchakato.

Mfumo huu humwezesha mwombaji kuingiza taarifa zake binafsi, za elimu na wadhamini. Ikumbukwe kutokana na mabadiliko ya teknolojia matumizi ya simu, sekretarieti imeboresha huduma na kuanzisha 'Ajira Portal mobile app' ambayo Watanzania wengi watapata taarifa za uwepo wa nafazi za kazi kwa haraka.

**SWALI: Vitu gani anatakiwa awe navyo mwombaji kama anataka kufungua akaunti katika mfumo huo?**

**JIBU:** Anatakiwa kuwa na baruapepe ambayo inatumika ili atakapotumiwa ujumbe uweze kumfikia, akijisajili kwenye mfumo, kuna ujumbe utatumiwa kwenye baruapepe kwa ajili ya kuipa uhai akaunti yake. Akifanya "account activation", ataweza kuingia kwenye akaunti ya Ajira Portal na anatakiwa kuingiza namba yake ya utambulisho wa taifa NIDA, nakala za vyeti vya taaluma na cha kuzaliwa vilivyohakikiwa na hakimu au wakili na picha.

**SWALI: Sekretarieti huendesha usaili kwenye vituo maalum, je, kuna mpango wowote wa kuwafikia watu wenye sifa katika mikoa na wilaya nchini kote?**

**JIBU:** Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha ambazo zimewezesha kufanyika kwa ujenzi wa mfumo wa kupima uelewa na ufahamu wa wasailiwa. Mfumo huu ambao uko katika hatua za mwisho za ujenzi utawawezesha wasailiwa kufanya mchujo kwa njia ya kidijitali katika vituo vilivyoko mikoani na wilayani wanakoishi.





# TAKUKURU yabaini upungufu bil. 5.2/- miradi ya maendeleo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, imefanya ufuatiliaji wa miradi 64 ya Sh. bilioni 27.7 na kubaini upungufu katika miradi 28 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.2.

Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Dodoma, John Joseph, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu.

Alisema upungufu umebainika katika miradi ya uezekaji wa majengo kwa kutumia mabati yasiyo na ubora, baadhi ya majengo kuwa na nyufa na wazabuni kulipwa fedha nyingi nje ya mkataba.

Alitaja upungufu mwingine kuwa ni wazabuni kulipwa fedha kabla ya kuwasilisha vifaa, kulipwa fedha na kuwasilisha vifaa pungufu na fedha za zuio kukatwa kwa makandarasi na kutowasilishwa katika mamlaka husika. "Mapungufu haya yamesababishwa kufunguliwa kwa majalada nane ya uchunguzi kwa baadhi ya miradi pamoja na kutoa ushauri kwa wasimamizi wa miradi,"alisema

Katika hatua nyingine alisema TAKUKURU imefanya utafiti 16 katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dodoma pamoja na warsha nne ambazo zilitumika kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa mifumo.

Alisema warsha tatu zimefanyika katika halmashauri ya jiji la Dodoma ambapo moja ilihusu udhibiti wa mianya ya rushwa katika huduma za ardhi.

Alisema warsha nyingine ilihusu mbinu za kuwezesha ufaulu katika shule za sekondari za kata na nyingine iulihusu ukusanyaji wa ushuru wa maegesho kwa vyombo vya moto.

"TAKUKURU Mkoa wa Dodoma katika kipindi cha miezi mitatu imefanikiwa kutoa elimu kwa wananchi kwa njia ya vipindi vya redio, ambapo timefanya jumla ya vipindi 40 na fursa ilikuwepo ya wananchi kuuliza maswali, kitoa ushauri na kujadili changamoto mbalimbali.

"Tumefanya semina 146 ambazo zimetumika kuongeza uelewa kuhusu rushwa na wananchi wameanza kuwa mabalozi wazuri wa mapambano dhidi ya rushwa. Tumeshiriki mikutano 116 ya hadhara ambayo changamoto mbalimbali zilijadiliwa na kupatiwa ufumbuzi,"alisema

Alisema katika kutekeleza program ya TAKUKURU Rafiki imewafikia kata 18 na kuibuka kero 130 kutoka sekta za elimu, afya, mifugo,maji,utawala,Tanesco, na polisi na kuzitafutia ufumbuzi.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miezi mitatu wamepokea malalamiko 165 ambapo kati ya hayo 53 hayakuhusu rushwa, hivyo walalamikaji 30 walielimishwa, huku malalamiko 10 yakihamishiwa jeshi la polisi na 13 walalamikaji walishauriwa kuyatatua.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kushoto), akipanda juu ya tangi la maji kwa ajili ya kuangalia mradi unaojengwa na Mamlaka ya Majisafi na Mazingira (DUWASA), Kata ya Zunguni jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC atoa siku 14 kukusanywa fedha za mbegu za alizeti

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali ametoa wiki mbili kwa maofisa Ugani, Watendaji wa Vijiji na Kata kukusanya fedha za mbegu za alizeti walizokopeshwa wakulima wa wilaya hiyo katika msimu wa kilimo wa 2022/2023.

Akizungumza juzi na watumishi hao alisema fedha hizo zipelekwe benki na stakabadhi za malipo wazipeleke katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

"Niwaambie tu hizo pesa mlizokusanya kwa wakulima hazitakuwa na msamaha tena kama ilivyokuwa kwenye msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022, kwani serikali iliona mbegu za ruzuku iliyotoa haikufanya vizuri," alisema.

Machali alisema kwa mujibu wa maofisa Kilimo wilaya hiyo inahitaji tani 1500 za mbolea na hadi sasa ni tani 447 zimefika kwahiyo bado kuna upungufu wa tani 1003.

Aidha,aliwasisitiza wakulima kila mmoja kuhakikisha anakuwa na kitambulisho cha Taifa ili kuepusha usumbufu unaojitokeza kwenye mfumo wakati wa kujisajiri kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku.

Mkuu wa Mkoa wa Singida ,Peter Serukamba, amewataka wilayani Mkalama kuongeza maeneo ya kilimo katika msimu huu wa kilimo ili kuongezea uzalishaji na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja wa wilaya na mkoa kwa ujumla.

Serukamba alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na uchumi mzuri pamoja na kusogeza huduma muhimu kwa wakulima ikiwepo pembejeo za kilimo ambapo aliwasisitiza kuendelea kujisajili katika daftari ili waweze kununua mbolea ya ruzuku kwa bei ya punguzo.

Aidha aliwataka kulima kilimo cha kisasa na chenye tija kwa kutumia mbolea pamoja na mbegu bora ili kuongezea uzalishaji. Serikali inaendelea kutatua kero mbalimbali za wananchi.

# Wasichana waongoza kufanyiwa ukatili wa kingono na ndugu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

ASILIMIA 38 ya wasichana wanafanyiwa ukatili wa kingono na ndugu au watu wa karibu katika mazingira ya nyumbani tofauti na wavulana ambao ni asilimia 13 katika Mkoa wa Singida.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa wajumbe wa mpango kazi wa taifa juu ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema utafiti uliofanywa nchini na The 2009 National Survey on Violence against Children umeonesha kuwa pia asilimia 73 ya wasichana na asilimia 72 ya wavulana wamefanyiwa ukatili wa kimwili na zaidi ya asilimia 60, wakibainika kufanyiwa na ndugu wa karibu huku wengine asilimia 40, hufanyika wakiwa shuleni.

Dk.Mganga alisema takwimu zinaonesha kuwa wanawake wenye umri miaka 15 hadi 49 waliofanyiwa ukatili wa kingono kimwili na kihisia na wenza wao mkoani Singida ni asilimia 45.

"Mpango kazi huu ulitengenezwa kwa njia shirikishi na ninayo imani kubwa kuwa kupitia mpango huu kila mdau atatambua wajibu wake na kuutekeleza ili tufikie malengo tuliyojiwekea ya kutokomeza ukatili dhidi wa wanawake na watoto kwa asilimia 50," ifikapo 2028," alisema.

Katibu Tawala huyo alisema siku 16 za kupinga Ukatili wa Kinjinsia kwa mwaka 2023, ziwe chachu kwa jamii kubadili sura ya vitendo vya ukatili Mkoa wa Singida ambao upo kati ya mikoa ambayo mimba, ndoa za utotoni na ukeketaji bado ni changamaoto kubwa.

Alisema katika kuhakikisha mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili yanafanikiwa, Dk. Mganga aliwataka wajumbe wa kamati hiyo watoe elimu kwenye taasisi na makundi mbalimbali.

Kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ni ya kimataifa, inayosimamiwa na kituo cha kimataifa cha Wanawake, tangu mwaka 1991, katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa na kuleta matokeo bora kwa jamii.

**Dk.Mganga alisema takwimu zinaonesha kuwa wanawake wenye umri miaka 15 hadi 49 waliofanyiwa ukatili wa kingono kimwili na kihisia na wenza wao mkoani Singida ni asilimia 45.**





# Watanzania washauriwa kutembelea vivutio utalii

**Na Nebart Msokwa,** RUKWA

WATANZANIA wameshauriwa kuwa na utamaduni wa kufanya utalii wa ndani kwa kutembelea vivutio vilivyopo nchini ili kujifunza, kufurahia na kusaidia kukuza pato la taifa.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Uhusiano wa Bodi ya Utalii, Augustina Makoye, wakati maofisa wa bodi hiyo walipofanya ziara kwenye Maporomoko ya maji ya Kalambo yanayotajwa kuwa ya pili kwa urefu barani Afrika.

Maofisa wa Bodi hiyo walitembelea kivutio hicho ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza na Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) ambapo wanahamasisha watanzania kutembelea vivutio na kuendeleza utalii wa utamaduni.

Augustina alisema utalii wa ndani ni muhimu kwa maendeleo ya taifa na kwamba kwa sasa wamewekeza nguvu kwenye uhamasishaji wa Watanzania kutunza utamaduni wao ikiwemo ngoma, vyakula vya asili pamoja na mila na desturi zingine.

Alisema mradi wa REGRO unalenga pia kuviwezesha vikundi mbalimbali vya utamaduni kwenye mikoa hiyo ya kusini ili vijue namna ya kuandaa vifurushi vyao na kuviuza kwa wageni wanaotembelea.

"Mikoa hii ya kusini ina vivutio vingi ambavyo ni vizuri sana, huu mradi wa REGROW, unalenga kuwasaidia Watanzania kuvijua vivutio hivi ili waweze kuvitembelea, lakini pia tunawezesha vikundi vya utamaduni kuimarisha kazi zao," alisema Augustina.

Mwongoza watalii katika Maporomoko ya Kalambo, Sadock Nsekela alisema maporomoko hayo yanavutia kwa kuwa na urefu wa zaidi ya mita 230 ambayo ndiyo marefu kuliko yote Afrika Mashariki. Alisema maporomoko hayo ni ya pekee kwa sababu yanatenganisha nchi mbili ambazo ni Tanzania na Zambia na kwamba Tanzania ina bahati kwa sababu maporomoko hayo yanaonekana vizuri zaidi upande wake.

Alisema kivutio hicho pia kipo jirani na Ziwa Tanganyika ambalo lina kina kirefu kuliko yote barani Afrika na hivyo ni rahisi mtalii yeyote kutembelea vyote kwa wakati mmoja.

"Kutoka kwenye maporomoko haya kwenda Ziwa Tanganyika pana urefu wa Kilomita nane pekee, mtalii anaweza kufurahia maporomoko haya na akaenda pia ziwani na akafurahia pia," alisema Nsekela.


Alisema miaka ya nyuma watalii walikuwa wanashindwa kukifikia kivutio hicho kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki lakini kwa sasa serikali imeboresha kwa kujenga ngazi ambazo zinatumika kushuka mpaka chini.

Kwa mujibu wa Nsekela kutoka juu kuna ngazi 1335 ambazo watalii wanazitumia kushuka ili kuyafikia maporomoko hayo na kwamba yapo maeneo manne ya kuyaangalia maporomoko hayo kwa ngazi tofauti.

Alisema eneo la kwanza maporomoko hayo yanaonekana kwa Asilimia 45, eneo la pili yanaonekana kwa asilimia 70, eneo la tatu ambalo limepewa jina la Dk. Hamis Kigwangala yanaonekana kwa asilimia 98 na eneo la mwisho maporomoko yanaonekana kwa asilimia 100.

Alisema maporomoko hayo yalitokea zaidi ya miaka milioni 25 iliyopita na yapo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki.

Mradi wa REGROW ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa Bodi ya Utalii kuweka uwiano sawa wa kutangaza vivutio vya utalii kati ya Kaskazini na Kusini mwa Tanzania aliyoyatoa kwenye maonyesho ya wakulima nanenane mkoani Mbeya mwaka huu.




Mshindi wa Sh. milioni 10 kupitia kampeni ya Vodacom Tanzania PLC inayoendelea ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha', Ester Skayanga (katikati), akishikilia mfano wa hundi aliyokabidhiwa na Masta Shangwe (aliyevalia kofia ngumu) pamoja Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa Vodacom, Happiness Shuma (wa pili kushoto), katika viwanja vya Uyole jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makangalawe waiangukia serikali ujenzi wa barabara

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WANANCHI wa Kijiji cha Makangalawe wilayani Makete mkoani Njombe wameomba serikali kuwafanyia ukarabati wa barabara yao ili kuwarahisishia kusafirisha mazao yao.

Wakizungumza na waandishi wa habari wananchi hao walisema barabara hiyo imekuwa changamoto hasa kipindi cha mvua.

"Kabla mvua hazijachanganya barabara ilikuwa inatumika vizuri,tunapata shida kwa kweli kama wakitutengenezea hii barabara hata uchumi wetu utakuwa vizuri," alisema Efeso Mgaya.

Reymond Chengula alisema barabara hiyo ni muhimu sana kwa uchumi wao kwa kuwa kiunganishi kikubwa cha wakulima na wafanyabishara wa mazao kama viazi,mbao na ngano.

"Tunaiomba serikali ituone wananchi wa kijiji cha Makangalawe inasaidia pia kutuunganisha na vijiji Jirani,vilevile kuna mapato mengi kwa sababu tunalima miti,viazi,ngano,wawekezaji wapo na mapato tunaingiza kila siku,"alisema

Mtendaji wa kijiji cha Makangalawe, Remijosi Magere, alikiri kuwepo kwa ubovu wa barabara hiyo na hivyo kunachangia kushuka kwa uchumi wa wananchi kwa kuwa wanashindwa kusarisha biashara zao kwa wakati kusudiwa.

Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini TARURA wilaya ya Makete,Mhandisi Frank Kapesa, aliwaahidi wananchi wa kijiji hicho kuwa wavumilivu kwani tayari serikali inafanya jitihada ili kufanya matengenezo.

Mhandisi Kapesa alisema kinachosababisha barabara zote kutotengenezwa kwa wakati ni bajeti kuwa ndogo ukilinganishwa na mahitaji yaliyopo.

"Tupo kwenye maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja kwa sababu hii barabara ni moja ya barabara zinazoombewa kufanyiwa maboresho, kwahiyo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha ujao tutaiingiza,kwa hiyo wawe tu na amani wananchi," alisema Kapesa.

**Wakizungumza na waandishi wa habari wananchi hao walisema barabara hiyo imekuwa changamoto hasa kipindi cha mvua.**

# Wanawake Njombe waonywa matumizi kemikali sehemu za siri

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAWAKE katika Halmashauri ya Mji Njombe, Mkoa wa Njombe, wameshauriwa kutotumia vitu vyenye kemikali ikiwamo sabuni katika kujisafisha sehemu za siri ili kuepuka magonjwa kwenye via vya uzazi.

Ushauri huo ulitolewa na tabibu kutoka kituo cha Best Hebalist Clinick, Agrey Alinani wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusiana na hatari ya matumizi ya vitu vyenye kemikali sehemu za siri kwa mwanamke .

"Kuna wanawake wengine wanajisafisha katika via vya uzazi kwa kutumia sabuni zenye kemikali,wanaosha mara kwa mara sehemu zao za siri kwa hiyo wanapata fangasi bila ya wao kujijua,"alisema Alinani.

Alinani alisema kuwa katika kuzingatia suala zima la usafi wanawake wanapaswa kujisafisha kutumia maji safi na salama bila ya kuweka kitu chochote.

"Wala wasiweke chochote kwa sababu kwa kufanya hivyo wataharibu bacteria ambao wanafanya via vya uzazi kuwa vizuri kwa hiyo ukitumia vitu vyenye kemikali unaondoa wale bacteria walinzi na wakiondoka wanakuja wale wabaya ambao wanaweza kuathiri," alisema Alinani.

Mmoja wanawake, Biana Mbawala alimweleza mwandishi wa gazeti hili kuwa kubwa ya wanawake kujisafisha kwa vitu vyenye kemikali kuwa ni kutokana na kupata changamoto ya kiafya bila ya kwenda kwa wataalamu wa afya. "Unakuta mtu anaumwa anatoka harufu mbaya bila ya kufikiria kwenda kwa wataalamu wa afya anapata ushauri mitaani kwamba tumia hiki harufu itakata basi anatumia kumbe anaongeza tatizo," alisema Biana Mbawala

Mary Sanga alitaja sababu nyingine kuwa ni wanawake kuamini kuwa wakitumia vitu hivyo watawaridhisha wanaume zao, pia ni kukosa elimu ya madhara ya kutumia vitu hivyo.

"Tatizo ni uelewa mdogo labda wanataka kuwaridhisha wanaume waonekane wapo vizuri huko sehemu za siri,wakati mwengine wanakamulia limao,wanaweka mavitu mengi lakini kuna madhara makubwa sana kwa sababu watu wa afya wanasisitiza kwamba huko chini hakutakiwi kuingia kitu chochote,"alisema Sanga.

Sanga alishauri wadau wa afya kuongeza kasi ya kutoa elimu juu ya madhara ya vitu hivyo kwa wanawake, kuwajengea uwezo ili waache kabisa kutumia.



## Vifo vya uzazi vyapungua, saratani ikipaa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua vimepungua katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, kutoka 70 kwa mwaka 2021 mpaka vifo 52 mwaka 2022.

Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla, aliyetaka kujua tathmini ya vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Waziri Mazrui alisema vifo vya watoto pia vimeshuka kutoka vifo 2,031 mwaka 2021 mpaka vifo 1,727 kwa mwaka 2022.

Akijibu swali jingine la mwakilishi huyo kuhusu tathmini ya maradhi ya saratani, Waziri huyo alisema maradhi hayo ya saratani kwa Zanzibar yapo na yanaongezeka kwa kasi.

Alisema kwa kipindi cha miaka tatu (2020, 2023) tathmini inaonyesha aina tano za saratani zinazoongoza, ambazo ni ya shingo ya kizazi waliogundulika 275, Saratani ya matiti 110, saratani ya tezi dume 126, saratani ya mfumo wa chakula 94 na Saratani ya kichwa na shingo ni 38.

Aidha akizungumzia kuhusu utaratibu wa utowaji wa leseni za wataalamu wa Afya, alisema hutolewa kupitia mabaraza ya wataalamu wa afya ambayo yameundwa kupitia sheria za wataalamu wa eneo husika zikiwemo; sheria namba 5 ya mwaka 2014 ya Baraza la Wauguzi na Wakunga.

Alitaja sheria nyingine kuwa ni namba 12 ya mwaka 1999 ya Baraza la Madaktari na Madaktari wa kinywa na meno, Sheria namba 10 ya mwaka 2020 ya Baraza la Wataalamu wa Maabaraza Tiba na Sheria nambari 15 ya mwaka 2012 ya Wataalamu wa afya na jamii na mazingira.

" Wizara kupitia Programu na vitengo imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi wa Afya kwa kufuata miongozo ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na kuzingatia mabadiliko na wakati uliopo," alisema.

Aidha, alisema mafunzo yanaendelea kutolewa kupitia programu za afya ya mama na mtoto, programu shirikishi ya Ukimwi, homa ya ini, kifua kikuu, ukoma, programu ya malaria sambamba na kusimamia watoa huduma na kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya.

Hata hivyo alisema utaratibu wa utoaji wa leseni kwa wataalamu wa afya wapya na wanaoendelea kutoa huduma umewekwa kwa mujibu wa sheria ya mtaalamu husika.

Mazrui alisema ufafanuzi wa utaratibu huo umeainishwa na masharti ya usajili wa utoaji leseni ikiwemo mfanyakazi lazima amalize masomo yake katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, awe amemaliza mafunzo tarajali (internship) katika hospitali ya kufundishia na awe amefaulu mtihani wa leseni unaotolewa na Baraza husika.

# Mpango wa utafiti wa miamba, madini waiva

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) imekamilisha mpango wa utafiti wa miamba na madini Zanzibar unaolenga kujua aina ya miamba iliyopo, sifa zake na aina ya madini yanayopatikana.

Waziri wa wizara hiyo, Hassan Shaibu Kaduara, amesema utafiti huo unatarajiwa kufanyika kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Novemba, mwaka huu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Amei, aliyehoji ni upi mkakati wa wizara kufanya utafiti wa uvumbuzi wa miamba ya madini hususan madini ya kimkakati ambayo yanaweza kutumika katika sekta za maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

Alisema Wizara kwa kushirikiana na kampuni ya Aseel Oil field Company Ltd inaendelea na utafiti wa awali kwa kisiwa cha Unguja ambapo utafiti huo umeshafanyika kwa Wilaya ya Kusini na unaendelea Wilaya ya Kati na kumalizia Wilaya zilizobaki kwa kisiwa cha Unguja kisha utafiti huo utafanyika kisiwani Pemba.

"Mheshimiwa Spika, taarifa zitakazopatikana kupitia tafiti hizo zitasaidia kujua aina za madini yaliyopo Zanzibar pamoja na kuwa na ramani ya kijiolojia ya Zanzibar"alisema.

Aidha, waziri huyo alisema utafiti huo utasaidia sekta nyinginezo ikiwemo sekta ya maji, ujenzi, mafuta na gesi asilia pamoja na udhibiti wa maafa na majanga ya asili ya kijiolojia.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC), Mwanaisha Ali Said na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili, wakitia saini makubaliano ya ushirikiano kati ya benki hiyo na Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC) yenye lengo la kuwawezesha wafanyakazi na wafanyabiashara kuweza kununua nyumba zilizoko kwenye miradi inayosimamiwa na shirika hilo visiwani Zanzibar, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Zanzibar kuwaondolea vikwazo wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema kwamba inaendelea kuwaondolea vikwazo watu wenye ulemavu ili kuleta mabadiliko na usawa katika shughuli zao za kila siku na kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Makamu wa Rais wa Kwanza Zanzibar, Othman Makamu Othman, aliyasema hayo juzi katika Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Watu wenye ulemavu Duniani yaliyofanyika katika Ukumbi wa Polisi Ziwani mjini Zanzibar .

Alisema miongoni mwa changamoto hizo kuwa ni kutowapo mazingira sahihi ya kuweka miundombinu rafiki ya barabara na majengo ya huduma ili nao wafaidike na huduma zinazotolewa.

Alisema serikali kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Watu kiuchumi inaendelea kuwapatia mitaji na mikopo isiyo na riba kupitia vikundi vya maendeleo ili kuwapa fursa ya kufanya biashara na kuendesha maisha yao.

Othman alisema katika kuhakikisha utekelezaji wa jitihada hizo unafanikiwa serikali imejenga dakhalia na Shule maalum zenye miundombinu mahsusi kwa kundi hilo huko katika eneo la Jendele Wilaya ya Kati Unguja pamoja na Pujini Kisiwani Pemba ambazo zinaendelea kutoa na kuimarisha ustawi wao wa huduma bora za elimu.

Alizitaka taasisi za serikali na wadau kuhakikisha wanaendelea kushirikiana hasa ili kupambana na umasikini, kupunguza njaa, kustawisha afya za watu, elimu bora , vifaa visaidizi , ajira zenye staha na kuondosha unyanyasaji wa kijinsia.

Aidha alisema ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapewa elimu ya kutosha ili kuishi salama bila maambukizo ya magonjwa ya kujamiiana ikiwemo virusi vya UKIMWI .

Makamu wa Rais alisisitiza ushirikianao huo pia yaelekezwe kuwalinda watu hao na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na kuhakikisha mazingira yanaimarishwa kwa lengo la kupunguza sababu zinazosababisha ulemavu.

Kaimu waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Nassor Ahmed Mazurui alisema siku hiyo ni makhususi katika kuzingatia suala la utu hasa kwa kuzingatia kwamba ulemavu sio mwisho wa ubinaadamu.

Alisema serikali inafanya jitihada kubwa kuweka mazingira na miundombinu rafiki katika kustawisha usawa na kupunguza vyanzo vinavyosababisha ulemavu ongezeko la walemavu nchini.

Akisoma risala mwakilishi kutoka Umoja wa vyama vya watu wenye ulemavu Zanzibar, Ali Omar, aliitaka serikali kupunguza masharti na vigezo vya mikopo kwa watu wenye ulemavu kwa kuweka masharti nafuu kwa jamii hiyo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JAQUELINE JOSEPH KYAI** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 152262 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 30/07/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **LR No: 485303/2023**

### KUPOTEA KWA CHETI



**MASANYIWA JOHN MASANYIWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S5027/0039 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MUGINI SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/NY//RB/420369/2022.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**GODFREY BASIL MWITUMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0751/118 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RUHUWIKO SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/10698/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MSHINDO ABDALLAH MSHINDO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 104 BRB. Chassis namba SKA167032533. Engine namba 35FEZ488CT. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8510/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY SHABANI HINANA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 488 DMT. Chassis namba NCP600067674. Engine namba 2NZ2573387. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8510/2023.**

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**
**(Made under the Registration of Documents Act, CAP. 117)**

BY THIS DEED I, FREDRICK MBERA BARAKA, alias FEDRICK MBERA BARAKA alias FREDRICK M. BARAKA alias FEDRICK MBERA NYAMHANGA of Kipunguni B. Machimbo Area, Ilala District, P.O. BOX 12519, Dar es salaam, do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former names of FEDRICK MBERA BARAKA alias FREDRICK M. BARAKA alias FEDRICK MBERA NYAMHANGA, as appear in my Form Four Leaving Certificate, my Form Four Academic Certificate (issued by National examination Council of Tanzania NECTA) and my National Identity Card No. 20000521141220000220 (issued by the National Identification Authority, NIDA) respectively, and in lieu thereof do assume as from the date hereto the name of FREDRICK MBERA BARAKA.

AND that the reason for change of name is that my birth certificates bears the name of FREDRICK MBERA BARAKA and when I joined Secondary School, form one, I was registered as FREDRICK MBERA BARAKA but in preparing my FORM FOUR leaving certificate the School misspelled my name as FEDRICK MBERA BARAKA instead of FREDRICK MBERA BARAKA while in preparing my form four Academic Certificate the National Examination Council of Tanzania (NECTA) spelled my name as FREDRICK M. BARAKA instead of FREDRICK MBERA BARAKA whereas initial "M" represent MBERA, further that in registering with the National Identification Authority (NIDA) I mentioned my name in the registration form as MBERA BARAKA NYAMHANGA as NYAMHANGA is my grandfather's name but in preparing National Identity Card the said Authority, NIDA, misspelled my names as FEDRICK MBERA NYAMHANGA instead of FREDRICK MBERA NYAMHANGA (my National Identity Card number is 20000521141220000220), hence needs to harmonize the documents with my birth certificate. AND in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereinafter in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of FREDRICK MBERA BARAKA as my name in lieu of the said names FEDDRICK MBERA BARAKA alias FREDRICK M. BARAKA alias FEDRICK MBERA NYAMHANGA.

AND with this Deed Poll I attach copies of the documents bearing the said names of FREDRICK MBERA BARAKA alias FEDRICK MBERA BARAKA alias FREDRICK M. BARAKA alias FEDRICK MBERA NYAMHANGA and the Affidavit as the names sworn on 16th August, 2023.





### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUDATADE ROMAN MBOWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 346 DEA. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/KIL/HAI/859/2023.**

### KUPOTEA KWA VYETI



**ALBERT GODFREY LUENA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0584-0042 kilichotolewa Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LWANDAI SEKONDARI mwaka 2008. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S2498-0525 kilichotolewa na NEEMA TRUST SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/49661/2023.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**LUKA CHRISTOPHER KIBASA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4724/0052 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NGANGWE SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/TAN/3251/2023.**

### KUPOTEA KWA VYETI



**MAULA SALESY KAGALI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1770/0032 kilichotolewa Baraza la Mitihani la Taifa kupitia IMAGE HIGH SCHOOL mwaka 2010. Cheti cha Chuo kilichotolewa na MEEP TRAINING COLLEGE mwaka 2013. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/49323/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIA JACOB SHAYO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 241 APG – TOYOTA CORSA. Chassis namba EL510071638. Engine namba AE1509371. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8169/2023.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**NOAH ABRAHAM JAPHET** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2196-0026 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia HEKA SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/7639/2023.**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Kicheko wanajeshi wa Afrika Mashariki kuondoka DRC

**KINSHASA,** DRC

RAIA wa mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wamefurahishwa na kitendo cha kuondoka kwa wanajeshi wa Kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACRF) na kwamba awamu ya kwanza imeanza na wanajeshi 100 wa Kenya walioondoka Mkoa wa Kivu.

Ilielezwa kuwa utekelezaji wa suala hilo ulianza juzi, huku raia wakieleza kuwa hatua hiyo italipa nguvu Jeshi la serikali ya Kongo kulitokomeza kundi la waasi wa M23 ambalo limekuwa likifanya mashambulizi na kushikilia maeneo kadhaa mashariki mwa nchi hiyo.

Ilibainishwa kuwa kundi hilo la kwanza la wanajeshi 100 wa Kenya liliondoka Kivu Kaskazini kupitia uwanja wa ndege wa kimataifa mjini Goma.

Askari hao waliokuwa wakishutumiwa na mashirika ya kiraia kushirikiana na kundi la waasi wa M23 wameondoka wakati hali ya usalama ikiendelea kuwa tete katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo.

Kabla ya wanajeshi hao kuondoka, kamanda wa Kikosi cha Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Francis Ogolla, aliwapongeza kwa kile alichosema wamepata mafanikio makubwa tangu kupelekwa kwao katika mkoa wa Kivu Kaskazini.

Wakati huo huo, kundi la M23 lilitangaza kuwa litachukuwa maeneo yote yaliyokuwa chini ya uongozi wa kikosi hicho cha kikanda. Huku mmoja wa wasemaji wa kundi hilo, Willy Ngoma (pichani chini), akithibitisha kuwa huo ndio mpango wa waasi hao, ambao utaanza kutekelezwa mara moja.

Kufikia asubuhi ya siku ya jana, iliripotiwa kuendelea kusikika kwa milio ya silaha nzito kwenye mji mdogo wa Malehe ulio umbali wa kilomita nane kutoka Sake.

Kwa mujibu wa mratibu wa asasi za kiraia wa wilaya ya Masisi, Telesphore Mitondeke, milio hiyo ilikuwa ni mashambulizi ya waasi wa M23 waliokuwa wanazilenga kwa makombora ngome za jeshi la Kongo.

Ilielezwa kuwa hofu ilikuwa imetanda katika mji wa Mushaki ambako mamia ya raia wameanza kukimbia nyumba zao kuelekea tena mji wa Sake ulio umbali wa kilomita 27 kutoka Goma. **DW**





Wananchi wa Palestina wakihuzunika baada ya kupoteza ndugu zao kutokana na shambulizi la Israel, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Zaidi ya raia 700 wauawa saa 24 zilizopita Gaza

**Na Maulid Mmbaga**

MAMIA ya Wapalestina wameuawa katika mashambulizi ya anga ya Israel katika muda wa saa 24 zilizopita huko Gaza huku Jeshi la Israel likiamuru raia kuhama maeneo zaidi ndani na karibu ya mji wa pili kwa ukubwa wa Khan Younis.

Mkurugenzi Mkuu wa ofisi ya vyombo vya habari vya serikali huko Gaza aliiambia Al Jazeera jana kwamba zaidi ya Wapalestina 700 wameuawa tangu Israel ianze tena mashambulizi ya mabomu baada ya mapatano ya siku saba kumalizika Ijumaa.

Inaelezwa kuwa zaidi ya watu milioni 1.5 wamekimbia makazi yao, wengi wao kutoka kaskazini mwa Gaza, tangu Israel ilipoanzisha mashambulizi ya kijeshi Oktoba 7 kufuatia shambulio baya la Hamas.

Inabainishwa kuwa usiku wa kuamkia jana mashambulizi makali ya mabomu yaliripotiwa katika miji ya Khan Younis, Rafah na baadhi ya maeneo ya kaskazini yaliyolengwa na mashambulizi ya anga na ardhini ya Israel.

Msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), James Elder alieleza kuwa "Kila mahali unapogeukia, kuna watoto walio na majeraha ya moto ya kiwango kikubwa, majeraha ya vipande, majeraha ya ubongo na mifupa iliyovunjika".

"Kinamama wanalia juu ya watoto ambao wanaonekana kama wako saa kadhaa kabla ya kifo. Inaonekana kama eneo la kifo hivi sasa," alisema.

Inabainishwa kuwa hospitali kuu ya Khan Younis ilipokea takriban watu watatu waliokufa na makumi kadhaa ya waliojeruhiwa kutokana na shambulio la anga la Israel ambalo lilishambulia jengo la makazi mashariki mwa mji huo.

Mfanyakazi wa utawala katika Hospitali ya Martyrs ya Al-Aqsa alibainisha kuwa miili ya watu 31 waliouawa katika shambulio la bomu la Israel katika maeneo ya kati ya ukanda huo ilipelekwa katika hospitali hiyo.

Kaskazini mwa Gaza, vikundi vya waokoaji vilivyokuwa na vifaa vidogo vilihangaika na kuchimba vifusi vya majengo katika kambi ya wakimbizi ya Jabaliya na vitongoji vingine katika Jiji la Gaza kutafuta manusura na maiti.

**Ndani ya Gaza, hakuna hoja ya msingi ya kwa nini madaktari wanafanya shughuli zao bila ya taa, na watoto kufanyiwa operesheni bila dawa ya kuwaondoa fahamu ili kupunguza maumivu.**

**VITA VYAENDELEA**

Licha ya kadhia hiyo, Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari, alisema jeshi hilo linapanua operesheni zake za ardhini katika Ukanda wa Gaza wakati idadi ya vifo vya raia wa Palestina ikitajwa kuongezeka, huku dalili mpya za mzozo zikienea katika eneo hilo.

Hagari alieleza kuwa Jeshi la Israel linafanya kazi popote pale ambako kundi la Hamas lina ngome. Ilielezwa kuwa wanajeshi wa Israel wamedhibiti maeneo kadhaa tangu mapigano yaanze, na kwamba baada ya muda wa kusitisha mapigano wa wiki moja kuisha, jeshi hilo limekuwa likijikita zaidi kwenye mashambulizi ya anga.

Kwa mujibu wa Shirika la Palestina la Wafa, mashambulizi ya anga yaliyofanyika jana kwenye lango la Hospitali ya Kamal Adwan, iliyoko kaskazini mwa Gaza, yalisababisha vifo vya watu kadhaa kwa huku serikali ya Hamas ikilishutumu jeshi la Israel kwa ukiukaji mkubwa wa sheria ya kimataifa ya ubinadamu.

Aidha, Israel inaishutumu Hamas kwa kuweka miundombinu ndani au chini ya hospitali na kutumia raia kama ngao.

Wizara ya Afya ya Hamas ilisema kwamba watu 15,523, huku asilimia 70 wakiwa wanawake na watoto, waliuawa tangu kuanza kwa mashambulizi ya Israel kwenye Ukanda wa Gaza, yaliyotekelezwa kujibu shambulio la umwagaji damu la Oktoba 7, mwaka huu la kundi la Hamas dhidi ya Israel.

**ICC**

Wakati hayo yakiendelea, mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), Karim Khan, alitoa wito kwa Israel, kuheshimu sheria za kimataifa za kivita.

Pia alisema anaongeza kasi ya uchunguzi wake wa ukiukwaji wa haki unaofanywa na walowezi dhidi ya Wapalestina huko Ukingo wa Magharibi.

"Ndani ya Gaza, hakuna hoja ya msingi ya kwa nini madaktari wanafanya shughuli zao bila ya taa, na watoto kufanyiwa operesheni bila dawa ya kuwaondoa fahamu ili kupunguza maumivu," alisema Khan.

Hata hivyo alisema wakati huu amekuwa muwazi kabisa wa kufuatwa kwa sheria na kama Israel haifuati sasa, isije ikalaumu baadaye. Vilevile Khan aliisisitiza Hamas, ambayo Marekani imeitangaza kuwa kundi la kigaidi, kuwa liheshimu sheria.

Israel, iliapa kulitokomeza kundi la Hamas, na kusema lengo lake ndani ya Gaza, ni kusambaratisha malengo yote ya kundi hilo, huku ikiwasihi raia kuondoka katika maeneo hayo.

***Chanzo mashirika ya kimataifa***

# SHIME AMALIZA KAZI TWIGA STARS KUIFURUSHA TOGO LEO

Na Saada Akida

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Wanawake Tanzania, (Twiga Stars), leo kina kibarua kigumu cha kulinda ushindi wake kwa kusaka sare ama kushinda kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Togo ili kukata tiketi ya kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (Wafcon), mwakani nchini Morocco.

Twiga Stars inashuka dimbani ikiwa na akiba ya mabao 3-0 waliyoyapata katika mchezo wa kwanza uliochezwa Desemba Mosi, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

**Tanzania leo inahitaji ushindi au sare yoyote katika mchezo huo ama kutokubali kufungwa kuanzia mabao 4-0 katika mechi hiyo ya marudiano, ili kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.**

Kuelekea mchezo wa leo, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, amesema maandalizi yameenda vizuri na matumaini yake makubwa ni kufanya vizuri na timu hiyo kujihakikishia tiketi ya kucheza fainali hizo.

Alisema wamefanyia kazi ubora wa Togo ikiwamo namna ya kuwazuia kufika kwenye eneo lao kwa kuwaandaa mabeki wake kuwa makini na kutowapa nafasi hiyo.

"Tumewaona jinsi wanavyocheza wanafika sana katika eneo la mpinzani hawaogopi, hilo tumemaliza, sasa kazi kubwa iko kwa vijana wangu kufanyia kazi yale tuliyowapa katika mazoezi na kusaka nafasi ya kufuzu kucheza fainali za Wafcon.

"Ninaimani kubwa na wachezaji wangu hasa kufanya vizuri katika mchezo huu kulingana na faida tuliyokuwa nayo ya ushindi tuliopata nyumbani na kilichobaki ni kumaliza dakika 90 za mwisho kwa kulinda ushindi wetu tuliopata nyumbani," alisema Shime.

Nahodha wa Twiga Stars, Oppa Clement, alisema benchi la ufundi limefanya majukumu yao na kazi iliyobaki ni kwao kupambana ili kutafuta matokeo chanya dhidi ya Togo kwa lengo la kukata tiketi za kucheza fainali hizo.

"Tuko tayari kukabiliana na wapinzani wetu, tunatambua umuhimu wa mchezo huu, hakuna tunachokihitaji zaidi ya kupambana kutafuta matokeo chanya ili kwenda kucheza fainali za Wafcon mwakani," alisema Oppa.

## TUNAPINGA...



Wanamichezo wa jogging wakiwa katika mbio za uzinduzi wa siku 16 za kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia Tandale maeneo ya Manzese, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Vodacom yatoa mamilioni Ngao ya Jamii Wanawake*

Na Saada Akida

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia makubaliano na Kampuni ya Mawasiliano ya Vodacom, kuwa sehemu ya mdhamini wa michuano ya Ngao ya Jamii kwa Wanawake wenye thamani ya Sh. milioni 50.

Mashindano ya Ngao ya Jamii kwa wanawake yanayoshirikisha timu nne, Bingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, JKT Queens akicheza dhidi ya Fountain Gate Princess na mechi ya pili ikiwa kati ya Simba Queens dhidi ya Yanga Princess, michezo hiyo itachezwa Uwanja wa Azam, Chamazi, Dar es Salaam Jumamosi wiki hii huku ule wa fainali ukipigwa Desemba 12, mwaka huu.

Michezo hiyo ni maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa ligi hiyo ambayo inatarajiwa kuanza Desemba 20, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Mashindano wa TFF, Baraka Kizunguto, alisema msimu huu wameboresha soka la wanawake kwa kuandaa mashindano ya Ngao ya Jamii.

Alisema mashindano hayo yatakuwa na mdhamini Kampuni ya Vodacom, ambayo imeingia makubaliano na TFF kwa kutoa zawadi kwa washiriki na kiasi cha fedha kwa timu hizo kwa ajili ya maandalizi ya mashindano hayo.

"Mechi ambazo zitachezwa ni JKT Queens ambao ni mabingwa watacheza dhidi ya Fountain Gate Princess huku Simba Queens wakivaana na Yanga Princess, michezo itakayochezwa Desemba 9 na 12, mwaka huu Uwanja wa Azam Complex.

"Timu zinatakiwa kujiandaa kwa sababu wadhamini wameandaa zawadi kwa washiriki wa mashindano hayo kila mmoja atapata kulingana na hatua atakayofikia," alisema Kizunguto.

Aliongeza kuwa TFF wanaendelea kufanya jitihada kwa soka la wanawake kupata wadhamini na kuifanya ligi hiyo kuendelea kuwa bora zaidi ya kuliko ilivyo sasa.

Naye Mkuu wa Uhusiano wa Vyombo vya Habari, Vodacom, Annette Kenora, alisema wamejikita katika soka la wanawake kwa kuanza kudhamini mashindano ya Ngao ya Jamii kwa kuwezesha timu pamoja na zawadi.

"Kwa kiasi cha Sh. milioni 50 ambazo tumeziweka katika mashindano hayo, milioni 2.5 zimetolewa kwa kila timu kwa ajili ya maandalizi, lakini bingwa atapewa zawadi ya milioni tano na mshindi wa pili milioni tatu, wa tatu atapewa milioni 1.5 na milioni kwa mshindi wa nne," alisema Annette.

# KLM yadhamini mashindano ya Tenisi Serengeti

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Ndege la KLM limejitolea kudhamini mashindano ya Tenisi ya 'McEnroe Serengeti Cup' yaliyopangwa kufanyika Ijumaa wiki hii.

Mashindano hayo makubwa yamepangwa kufanyika ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti mkoani Mara.

Tukio hilo la kipekee linalenga kuutangaza mchezo wa tenisi nchini Tanzania pamoja na fursa ya kipekee ya kuchunguza mandhari ya kuvutia ya Serengeti.

Akizungumza jana kuhusu mashindano hayo, Meneja wa Shirika hilo kwa Ukanda wa Afrika Mashariki, Kusini na nchi za Nigeria na Ghana, Marius Van der Ham, alisema ushiriki wa Rais Samia Suluhu Hassan katika kutangaza utalii wa Tanzania umeongeza hali ya heshima na sifa ya vivutio vya Tanzania.

Alisema kwa watu wa Tanzania, mashindano haya ya kusisimua yanakuja na faida nyingi, ikiwa ni pamoja na nafasi ya kushirikiana na baadhi ya wachezaji bora wa tenisi duniani, kuwahamasisha zaidi vijana kutafuta fursa zaidi ya waliyoizoea.

"Kama Shirika la Ndege la Kimataifa, tunaelewa athari kubwa ya kuunganisha watu, tamaduni na ndoto ambazo zimekuwapo Tanzania kwa miaka 54 sasa. Tunatambua hasa nguvu ya michezo katika kukuza umoja na msukumo, hasa miongoni mwa vijana," alisema Van Der Ham.

Alisema sehemu ya mapato yatakayopatika katika mashindano hayo yatatolewa kwa jamii.

Alisema KLM kama mfadhili wa mashindano hayo inaonesha kujitolea kwa shirika hilo katika kuunga mkono mipango ya kipekee na yenye matokeo inayofanywa na Serikali ya Tanzania na kuunganisha watu na tamaduni mbalimbali ulimwenguni.

Alisema mashindano hayo yatavutia wapenzi na mashabiki wa mchezo huo duniani kote.

**Kama Shirika la Ndege la Kimataifa, tunaelewa athari kubwa ya kuunganisha watu, tamaduni na ndoto ambazo zimekuwapo Tanzania kwa miaka 54 sasa.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MULLER AHUSISHWA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na Ujerumani, Thomas Muller mwenye umri wa miaka 34, amehusishwa na uhamisho wa Manchester United baada ya kutakiwa na nahodha wa zamani wa klabu hiyo ya 'Bavaria', Lothar Matthaus, kutafuta muda wa kucheza kwingineko. ***(The sun)***

### SOULE AVUTIWA JUVE

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Matias Soule, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Frosinone anavutiwa na Ligi Kuu ya England, huku Newcastle United ikiongoza mbio za kumnasa Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Gazetta dello Sport)***

### SANCHO KUUZWA JUVE

KLABU ya Manchester United inaweza kuwauza kiungo wa kati wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 na kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek (26), kwa Juventus kwa pauni milioni 26. ***(The Sun)***

### GREENWOOD AJADILIWA UTD

SIR Jim Ratcliffe, ambaye bado hajakamilisha mpango wa kuchukua shughuli za soka ndani ya Klabu ya Manchester United, tayari yuko kwenye majadiliano kuhusu mustakabali wa mshambuliaji, Mason Greenwood, 22. ***(Caught Offside)***

### TODIBO KUNG'OLEWA NICE

BEKI wa kati wa Ufaransa na Nice, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23, anawaniwa na Manchester United. ***(Sky Sports Germany)***

### KUREJESHWA ATLETICO

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo, amesema fowadi wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24, atarejea katika klabu hiyo ikiwa Barcelona wataamua kutofanya uhamisho wake wa mkopo Nou Camp kuwa wa kudumu. ***(Goal)***

### MAINOO MSHAHARA JUU

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Kobbie Mainoo mwenye umri wa miaka 18, ataongezewa mshahara wake kutoka pauni 10,000 hadi 20,000 kwa wiki ikiwa atakuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza. ***(Star)***

### WACHEZAJI KUOMBA FIDIA

BAADHI ya wachezaji wa Everton wanaweza kuomba fidia kutoka klabu hiyo kwa kupoteza mapato yao iwapo watashuka daraja, kutokana na adhabu ya pointi 10 ya 'Toffees' hao kwa ukiukwaji wa kanuni za fedha. ***(The sun)***

### FOREST NA VIKWAZO

KLABU ya Nottingham Forest inaweza kukabiliwa na vikwazo vya uhamisho wa Januari juu ya malipo ya ada ya kuchelewa inayodaiwa na mawakala. ***(The Sun)***

### WEST HAM KUONGEZA UWANJA

KLABU ya West Ham inatazamiwa kutuma maombi ya kuongeza uwezo wa Uwanja wa London hadi kubeba watu 68,000 siku za mechi, jambo ambalo litaufanya kuwa uwanja wa pili kwa ukubwa kwenye Ligi Kuu nyuma ya Old Trafford. ***(The Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND HATARINI KUADHIBIWA NA FA

**MANCHESTER,** England

**Mwamuzi alisema cheza na baada ya kutoa pasi, alisimamisha mchezo, sitaki...**

ERLING Haaland anaweza kuadhibiwa na Chama cha Soka cha England (FA), kwa kumkosoa mwamuzi, Simon Hooper, wakati Manchester City ikitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Tottenham Hotspur juzi na chapisho lake kwenye mtandao wa X (zamani twitter).

**Bao la kichwa la Dejan Kulusevski dakika ya 90 liliipa pointi Spurs, lakini City walinyimwa nafasi ya kushinda dakika tano baada ya zile za lala salama wakati mwamuzi Hooper aliposimamisha mchezo huku Jack Grealish akielekea kufunga kwa pasi ya Haaland.**

Haaland alichezewa vibaya na beki wa Spurs, Emerson Royal, katikati ya uwanja, lakini akanyanyuka na kumpasia Grealish. Mwanzo mwamuzi Hooper aliashiria faida kwa Man City kuendelea kushambulia, lakini kisha akapuliza filimbi wakati Grealish alionekana kuwa tayari kufunga.

Uamuzi huo ulizua hasira kutoka kwa Haaland, ambaye alioneshwa kadi ya njano na Hooper, lakini fowadi huyo wa Norway sasa yuko katika hatari ya kuadhibiwa na FA kwa chapisho lake kwenye X kwa kukiuka kanuni E3.1, inayosimamia maoni ya mitandao ya kijamii au matamshi yanayotolewa kwenye vyombo vya habari.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alishtakiwa na FA kwa maoni aliyoyatoa mwamuzi wa mechi kutokana na kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Newcastle mwezi uliopita. ESPN imewasiliana na FA kuuliza ikiwa Haaland pia atapokea adhabu.

Kocha wa City, Pep Guardiola alisema tukio hilo si sababu ya timu yake kupata sare kwenye mchezo huo, huku akimtetea Haaland.


"Ni kawaida," Guardiola alisema. "Maoni yake yalikuwa yale yale kwa wachezaji 10. Kanuni ni kwamba huwezi kuzungumza na waamuzi au maofisa wanne, kwa hiyo tulipaswa kuwa na wachezaji 10 waliotolewa kwa kadi nyekundu. Amesikitishwa kidogo.

"Hata mwamuzi - kama angeichezea Man City leo (juzi) angesikitishwa na kitendo hicho, hilo ni la uhakika.

"Nafanya makosa, wachezaji hufanya makosa. Erling alipoanguka, mwamuzi alisema cheza na baada ya kutoa pasi, alisimamisha mchezo.

"Sitaki kumkosoa, lakini hatukupata sare kwa ajili hiyo."

# NEVES AKATAA KUONDOKA SAUDI ARABIA




**RIYADH,** Saudi Arabia

KIUNGO wa kati wa Al Hilal, Ruben Neves, amesisitiza kuwa anataka kubaki na timu hiyo ya Saudi Arabia licha ya kutakiwa na Arsenal na Newcastle United.

Neves, ambaye aliondoka Wolverhampton Wanderers majira ya joto, kuna timu nyingi kwenye Ligi Kuu England zinazomwania.

Newcastle awali walionesha nia ya kutaka kumsajili Neves kwa mkopo, lakini sasa wamefikiria kumsajili kiungo huyo wa Al Hilal kwa mkataba wa kudumu.

Arsenal pia ni miongoni mwa timu zinazomfuatilia Neves, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ameweka wazi kuwa hataki kurejea England.

Alipoulizwa kama kuhamia Newcastle Januari kunawezekana, Neves aliiambia BBC Sport: "Siendi."

"Nadhani huo ni uvumi kwa sababu ya mmiliki wa klabu na shaka kwa sababu nimecheza England pia.

"Kulikuwa na nia ya Newcastle kabla sijaja hapa, lakini nina furaha sana hapa, familia yangu ina furaha sana, kwa hiyo nina wakati mzuri."

"Kila kitu kinaenda vizuri sana kwangu na ninataka kubaki hapa."

Al Hilal, inayomilikiwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudia (PIF), ambao wanamiliki Newcastle, walimsajili Neves kwa pauni milioni 47 wakati wa majira ya joto na wamemshuhudia akicheza mechi 19, akiiongoza timu yake kileleni mwa Ligi Kuu ya nchini hiyo.

Kuhamia kwake Mashariki ya Kati kulikuja kwa mshtuko mkubwa kwani Neves mwenye umri wa miaka 26, alikuwa anatakiwa na timu nyingi za Ulaya huku Liverpool na Barcelona wakifuatilia kupatikana kwake kabla ya kiungo huyo kuondoka Molineux.

# *Felix: Nimepata furaha kuifunga Atletico*

**BARCELONA,** Hispania

JOAO Felix amesema utulivu ulichochea yeye kushangilia baada ya kufunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 wa Barcelona dhidi ya klabu yake ya Atletico Madrid, Jumapili.

Baada ya kupachika bao dakika ya 28, Felix alishangilia kwa kunyanyua mikono juu katika Uwanja wa Olympic mbele ya mashabiki wa Atletico.

Fowadi huyo wa Ureno alijiunga na Barca kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Atletico mnamo Septemba na alisema kushangilia huko kulihusiana na nyakati ngumu kabla ya kupata uhamisho huo.

"Ilikuwa ya kuvutia," alisema Felix akinukuliwa na Movistar baada ya mchezo.

"Mwisho wa siku, uko kwenye joto la mchezo na ilikuwa hisia ya ahueni kwa kila kitu nilichopitia wakati wa majira ya joto.

"Ni wale tu walio karibu nami, hasa familia yangu, wanajua niliyopitia. Hii ilikuwa kwa ajili yao; nilihisi faraja kwa ajili yao pia."

Mwendelezo wa mchezo ulikuwa umetawaliwa na vita vya maneno kati ya Felix na baadhi ya wachezaji wenzake wa zamani.

"Ninaishi nao vizuri," aliongeza. "Wanajua haina uhusiano wowote nao. Sina chochote dhidi yao. Natumaini mambo yatawaendea vizuri, sio dhidi yetu.

"Kila wiki kunazungumzwa juu yangu, kwa uzuri au kwa ubaya. Ninazingatia kazi yangu, bila kuangalia kile ambacho watu wanasema au kufikiria. Ninafanya kazi ili kuimarika na kuwa mchezaji bora."

Bao lake dhidi ya Atletico lilikuja siku nne tu baada ya kufunga dhidi ya FC Porto kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki.

Ilikuwa ni mara yake ya tano msimu huu kwa Barca na kuwafungia 'Blaugrana' katika ushindi muhimu, na kuwasogeza mbele ya Atletico kwenye msimamo wa ligi, pointi nne nyuma ya viongozi Real Madrid na Girona.

"Kwa mara nyingine alileta mabadiliko kwa timu," alisema Kocha wa Barca, Xavi Hernandez katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Alifanya kazi kwa bidii, akashinda mipira mingi nyuma, alikuwa mzuri sana kwenye nafasi na ana maelewano mazuri na Joao Cancelo.

"Nimefurahishwa naye. Ana furaha na analeta mabadiliko katika michezo, jambo ambalo ni la ajabu kwake. Ilikuwa ni utendaji wa akili kwa sababu wakati mwingine ukiwa na motisha unaweza kufunga kirahisi."




# Klopp akunwa na kiwango Liverpool

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp alisifu "mabao mazuri" yaliyofungwa na timu yake ya Liverpool wakati ikitoka nyuma na kuifunga Fulham kwenye Uwanja wa Anfield Jumapili.

'Wekundu' hao walikuwa mbele mara mbili, lakini vijana wa kocha Marco Silva wakawapiku na kuongoza kwa mabao 3-2.

Lakini mabao ya dakika za lala salama kutoka kwa Wataru Endo na Trent Alexander-Arnold, yaliwapa wenyeji pointi zote tatu na Klopp alifurahishwa na kiwango cha ushambuliaji cha wachezaji wake.

Alisema: "Sidhani kama nimewahi kuona mchezo wenye idadi hii ya mabao mazuri.

"Tulifunga mabao ya ajabu leo (juzi). Kipindi cha kwanza tayari tulitoa mabao, ulinzi ulikuwa mbaya. Lakini hiyo ni soka, soka inaamuliwa kwa undani na hali hizi huchukua kasi."

Licha ya Liverpool kukosa uimara wa safu ya ulinzi, bado waliweza kutawala mchezo na kutengeneza mashuti 26 na kumiliki mpira kwa asilimia 62.

Klopp aliongeza: "Kwa kweli tulikuwa wazuri kwenye mchezo, tulicheza vizuri. Tulikuwa na nafasi kubwa, ni wazi, lakini hatukuzitumia na hiyo inawaweka hai, lakini mwisho wa mchezo tulion-doka na ushindi."



# MWANA FA ‘ANOGESHA’ TAMASHA LA EXIM BIMA FESTIVAL, ATOA NENO

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, ametoa wito kwa Kampuni za Bima na Taasisi za Fedha nchini kuongeza ufadhili wao kwenye sekta ya michezo ili kuchochea ukuaji wa sekta hiyo inayokua kwa kasi.

**Mwana FA alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati alipopata fursa ya kupamba msimu wa kwanza wa Tamasha la Bima Festival lililoratibiwa na Benki ya Exim Tanzania ambapo aliziomba taasisi hizo kubuni huduma mbalimbali zinazolenga kuwasaidia wadau wa sekta ya michezo na burudani nchini.**

Katika tamasha hilo lililoratibiwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wa sekta ya bima nchini zikiwamo Kampuni za Alliance Life Assurance Limited, Alliance Insurance Corporation Limited, Jubilee Allianz General Insurance Company Limited, Strategis Insurance Company Limited, The Heritage Insurance Tanzania na kampuni wateja wa benki hiyo ikiwamo Kampuni ya bidhaa za Plastic ya CELLO pamoja na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Taifa Mining, ilishuhudiwa timu ya mpira wa miguu ya Exim ikiibuka mshindi wa jumla kwenye mashindano ya mpira wa miguu yaliyohusisha wadau wote.

Akizungumza wakati akizindua tamasha hilo Mwana FA pamoja na kuwapongeza wadau hao kwa kuandaa tukio hilo lililotoa fursa ya kufurahia pamoja, kubadilishana mawazo na kujengeana ufahamu zaidi kuhusu huduma zao, aliwasihi wajitokeze zaidi kuunga mkono shughuli mbalimbali zinazofanywa na wadau wa michezo na burudani nchini kwa kudhamini shughuli zao mbalimbali na kuwatumia kwenye hamasa za kibiashara yakiwamo matangazo.

“Mchango wenu unaweza kutafsiriwa katika maeneo mengi ya kimichezo, lakini msisitizo wangu nauweka zaidi katika udhamini wa matukio mbalimbali ya michezo hususan katika uibuaji wa vipaji na kusaidia klabu mbalimbali zinazoshiriki ligi mbalimbali hapa nchini ikiwamo Ligi Kuu. Zaidi pia niwaombe muendelee kubuni huduma za bima na huduma za kifedha mahususi kwa wanamichezo na wasanii ili muwasaidie kulinda afya na kazi zao na zaidi kuwajenga kiuchumi,” alisema.

Mwana FA alipongeza benki hiyo kwa jitihada zake za kukuza michezo hapa nchini kupitia msaada wa vifaa vya michezo inavyotoa kwa shule za msingi na sekondari katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

“Mmeonesha dhamira na nia njema ya kuinua vipaji vya vijana na kuwezesha maendeleo ya michezo nchini. Tunatambua mchango wenu mkubwa katika kuendeleza michezo na tunawashukuru kwa kuwa wabia wetu katika kufanikisha malengo yetu ya kitaifa katika sekta hii,” alisema huku pia akionesha matumaini makubwa kuwa Tamasha la Exim Bima Festival litakuwa na mafanikio makubwa na litaleta matunda yaliyotarajiwa.

Awali, akizungumza kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Mkuu wa Idara ya Uwekezaji Kimkakati na Matawi ya Nje wa benki hiyo, Sumit Shekhar, alisema kupitia tamasha hilo litakalokuwa likifanyika kila mwaka, benki hiyo imejipanga kutumia vema fursa ya michezo na burudani kuboresha mahusiano yake na wadau wake mbalimbali wakiwamo wateja, wadau wa bima, wafanyakazi, mamlaka mbalimbali zinazosimamia sekta ya bima na benki pamoja na serikali.

“Tukiwa kama wadau muhimu wa sekta ya fedha na bima nchini kupitia huduma yetu ya bima ijulikanayo kama ‘Bima tu Malipo Tuachie’ tumejipanga kuhakikisha tunalitumia vema tamasha hili kama mkakati muhimu wa kuboresha mahusiano baina yetu na wadau wetu tukiamini mahusiano ndio nguzo ya kwanza kwenye biashara yoyote na Tamasha la Exim Bima Festival linakuja kama namna bora ya kutusaidia kufanikisha hilo,” alisema Shekhar.

Akizungumzia ushindi wa jumla katika mashindano ya mpira wa miguu baina ya wadau hao, mfungaji bora katika mashindano hayo, Calvin Kilua kutoka timu ya Benki ya Exim, alisema siri ya mafanikio ni timu yake kujiandaa vema kwa ajili mashindano hayo sambamba na kutafsiri vema maelekezo ya kocha wa timu hiyo ambaye ni Meneja Rasilimali Watu, Mikidadi Ngoma.

“Baada ya mafanikio haya tunaamini kwamba tamasha lijalo litahusisha timu nyingi zaidi na ushindani utaongezeka. Hivyo tutaendelea kujiweka sawa kwa mazoezi zaidi kwa kuwa mazoezi pia ni afya na ukizungumzia afya ni moja ya agenda ya msingi kwenye huduma zetu za bima,” alisema Stanley Kafu, Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim.

## Bara, Kenya U-18 nusu fainali ya kibabe leo

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya soka wavulana ya Tanzania Bara leo itajitupa katika Uwanja wa Jomo Kenyatta, Kisumu nchini Kenya, kucheza na wenyeji wao hao kwenye mechi ya nusu fainali ya michuano ya kusaka ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati Ukanda wa CECAFA chini ya miaka 18.

Bara ilitinga hatua hiyo baada ya kushika nafasi ya pili kwenye Kundi B ikikusanya pointi nne, katika kundi ambalo liliongozwa na Uganda iliyomaliza na pointi sita.

Wakati Bara, ikicheza nusu fainali ya kwanza, Uganda itacheza nusu fainali ya pili dhidi ya Rwanda iliyomaliza Kundi A ikiwa nafasi ya pili na pointi zake sita, huku Kenya ikiwa kinara wa kundi hilo kwa pointi tisa.

Fainali ya michuano hiyo inatarajiwa kuchezwa Ijumaa kwenye uwanja huo huo.

Kocha Mkuu wa Bara, Habib Kondo, amesema mechi itakuwa ngumu kutokana na timu zote kuonekana kucheza soka linalofanana, lakini wamejiandaa kukabiliana na wapinzani wao ambao watakuwa wako nyumbani wakipata sapoti kutoka kwa mashabiki wao.

Moja kati ya mambo ambayo ni gumzo kwenye michuano hiyo ni timu ndugu za Bara na Zanzibar zilizokuwa kundi moja kufanana kila kitu, lakini Bara ikafuzu nusu fainali kwa kanuni.

Kanuni iliyotumika ni Bara kuwa na kadi chache za njano, huku kila timu ikiwa imecheza mechi tatu, ikishinda moja, sare moja na kupoteza moja, mabao matatu ya kufunga na kufungwa, zote pia zikimaliza na pointi nne.



Kikosi cha Timu ya Benki ya Exim kilichoibuka mshindi wa jumla kwenye mashindano ya mpira wa miguu yaliyohusisha wadau wote wakati wa Tamasha la Exim Bima Festival lililoratibiwa na benki hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Benchikha aahidi kuibadilisha Simba*

INATOKA UKURASA 24

kwenye mechi hiyo dhidi ya Wydad.

Alisema wachezaji wanatambua umuhimu wa mchezo huo, na kwamba wanahitaji kufanya vizuri kwa sababu malengo yao ni kuona Simba inasonga mbele kuvuka makundi na kucheza robo fainali.

“Samahani mashabiki wetu, tusahau matokeo yaliyopita ambayo kocha wetu (Abdelhak Benchikha) amefanyia kazi mapungufu yetu sasa nguvu na akili zetu tumezielekeza kusaka ushindi dhidi ya Wydad Casablanca,” alisema Baleke.

Kuhusu tetesi za kutakiwa kurejea katika klabu yake ya TP Mazembe, Baleke alisema bado yupo na ni mtoto wa Simba, anachokifikiria zaidi ni kuona timu yake inafanikiwa kuvuka katika hatua ya makundi na kwenda robo hatimaye nusu fainali.

Simba wanatarajia kushuka dimbani Desemba 9, mwaka huu, wakiwa ugenini dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco, mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Grand stade de Marrakech, uliopo Marrakech, saa 4:00 usiku.

## Serikali yacharuka

INATOKA UKURASA 24

merudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yao kwa ajili ya kwenda kupambana kusaka alama muhimu katika mchezo ujao.

Alisema Medeama ni timu iliyokuwa imara na wanatakiwa kuwa makini kuanzia safu ya ushambuliaji na ulinzi kuhakikisha hawaruhusu kufungwa na kutumia vizuri nafasi zinazopatikana.

“Tunaendelea kusahihisha makosa yetu, tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi yetu dhidi ya Medeama, wapinzani wetu ni wazuri na tunatakiwa kuwa makini hasa nafasi tunazotengeneza kuzitumia ipasavyo.

Michezo

Jumanne Desemba 5, 2023

Nipashe



Klopp akunwa kiwango Liver

UKURASA 22

IKO HIVI...



Wachezaji wa Yanga wakifanya mazoezi ya viungo kujiandaa na mechi ijayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini dhidi ya Medeama ya Ghana itakayopigwa nchini humo Ijumaa wiki hii. **PICHA: YANGA**

## Serikali yacharuka mashabiki wang'oa viti Yanga, Al Ahly

**Na Saada Akida**

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, imeeleza kukerwa na kitendo cha baadhi ya mashabiki kuharibu miundombinu ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati wa mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Yanga na Al Ahly ya Misri iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1, Jumamosi iliyopita.

Katika mchezo huo ambao Yanga ilitangulia kufungwa, baada ya kusawazisha dakika za mwisho, baadhi ya mashabiki walionekana waking'oa viti uwanjani hapo na kuanza kuvirusha kwa wapinzani wao.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, mbali na kukemea vitendo hivyo vya uharibifu wa miundombinu ya viwanja vinavyofanywa na baadhi ya mashabiki wakati wa kushangilia timu zao, amesema hatua zitachukuliwa dhidi ya waharibifu hao.

Mwana FA alisema tukio la uharibifu lililojitokeza kwenye mechi hiyo uchunguzi unaendelea kufanywa na watakaobainika watawajibika kulipia uharibifu huo.

"Ni kweli nimeona video ya tukio hilo kama ambavyo viti vilishawahi kung'olewa pale na watu wakalipishwa kufanya ukarabati ule hakuna kitu kitabadilika, tunafanya uchunguzi ukikamilika wahusika wote watalipia," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameigeukia safu yake ya ushambuliaji kuhakikisha wanakuwa makini kutumia nafasi zinazopatikana hasa kuelekea mechi yao ya tatu ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama ya Ghana.

Amesema mechi iliyopita walishindwa kutumia nafasi walizozitengeneza, hivyo ameanza kulifanyia kazi haraka kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Medeama Ijumaa wiki hii.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamond alisema baada ya mechi dhidi ya Al Ahly, wa-

INAENDELEA UKURASA 23

# Benchikha kuibadili Simba

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

● ● ● Aanika mifumo anayotaka kuelekea kwa Wydad, Baleke naye awatuliza mashabiki, asema...

WAKATI kikosi cha Simba kilirejea jana kambini kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa tatu wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco, Kocha Mkuu wa kikosi hicho Abdelhak Benchikha ameahidi kuibadilisha timu yake icheze kama anavyotaka yeye.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo aliyejiunga hivi karibuni akitokea USM Alger ya Algeria, amesema kwa jinsi alivyokiona kikosi chake bado kuna mambo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na kitabadilika.**

"Tunalazimika sasa kushinda kwenye mechi zetu zinazofuata, na kufunga mabao mengi pia, nilichofurahi kwenye mechi iliyopita ni mabadiliko kidogo kwa wachezaji wangu, lakini kuna tatizo kwenye uamuzi, na kuna mambo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na kuyabadilisha ili kuendana na muundo wa soka la kisasa, hili nitaanza kulifanyia kazi mazoezini," alisema kocha huyo ambaye mpaka Simba inacheza mechi ya raundi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi Jwaneng Galaxy nchini Botswana Jumamosi iliyopita hakuwa ameifundisha timu hiyo zaidi ya siku tatu.

Kocha huyo alisema anataka kutengeneza timu itakayocheza mifumo tofauti, kujiamini, kasi inapoingia kwenye eneo la hatari pamoja na kufanya uamuzi sahihi kwa wakati sahihi," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba pamoja na kwamba timu yao ilitoka suluhu, lakini wameonekana kuridhishwa na uchezaji wa timu yao, huku wakienda mbali zaidi kwamba tangu msimu huu uanze katika mechi zote za kimafaifa na Ligi Kuu, wachezaji wa timu hiyo kwa mara ya kwanza wamecheza kwa kiwango cha kuridhisha, hivyo wengi kuwa na imani na kocha huyo kama akikaa na kuifundisha kwa muda mrefu kidogo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema kikosi kilitarajia kuanza mazoezi jana saa tisa kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam na moja kwa moja kuingia kambini kwa ajili ya mechi dhidi ya Wydad Casablanca inayotarajiwa kucheza Jumamosi kwenye Uwanja wa Marrakech nchini Morocco.

"Tuliporejea tuliwapa mapumziko kidogo wachezaji wetu, lakini wanarejea leo (jana), saa tisa na kuanza rasmi mazoezi na kambi kwa ajili ya mechi ya tatu dhidi ya Wydad, ni mechi ngumu kwa sababu jamaa wamepoteza zote mbili za mwanzo, hivyo watataka kuamkia kwetu, lakini na sisi tunajipanga, kwa siku hizi kadhaa nadhani kocha wetu atapandikiza ujuzi na ufundi wake kwa wachezaji.

"Tumeona siku chache tu baada ya kuichukua timu kuna kitu kimeanza kuonekana, nadhani baada ya muda kidogo timu itakuwa sawa, umeona wachezaji wanajituma, wanakimbia, na hata utimamu wa mwili umeanza kuongezeka," alisema Ahmed.

Asec Mimosas inaongoza Kundi B, ikiwa na pointi nne na mabao mawili, sawa na Jwaneng Galaxy inayoshika nafasi ya pili, lakini yenyewe ina bao moja, Simba ikiwa namba tatu kwa pointi mbili na Wydad ikiburuza mkia bila pointi.

Wakati huo huo, mshambuliaji wa timu hiyo, Jean Baleke amewashusha presha mashabiki wa timu hiyo na kusema bado wananafasi ya kusonga mbele kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakapoenda kusaka alama tatu dhidi ya Wydad Casablanca.

Amesema hadi sasa wana pointi mbili na wanaimani kubwa ya kupata pointi tatu za mchezo dhidi ya wenyeji wao, Wydad Casablanca ugenini ili waweze kufikisha pointi tatu muhimu kwa ajili ya kufikia malengo yao.

Akizungumza na Nipashe jana, Baleke aliwaomba msamaha mashabiki wa Simba kwa matokeo ya nyuma na kuwataka kuungana kuwa nguvu mmoja kuelekea

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >